# ATHARI ZA SHENG KATIKA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI MJINI KISII: UTAFITI KIFANI WA SHULE ZA UPILI ZA GUSII HIGHLIGHTS NA DARAJA MBILI.

**NA**

**LYDIAH NYAMBEKI MEKONGE**

**C50/67010/2013**

**IDARA YA KISWAHILI; CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**2016**

## Ungamo

**Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijatolewa katika chuo kingine chochote nchini Kenya.**

***Sahihi*____________________________ *Tarehe* _____________________________**

**Mekonge nyambeki lydiah (Mtahiniwa)**

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.**

***Sahihi* _______________________ *Tarehe* ____________________**

**Dkt. Ayub Mukhwana (Msimamizi)**

***Sahihi* _________________________ *Tarehe* ____________________**

**Dkt. Prisca Jerono (Msimamizi)**

## Shukrani

Ningependa kuwashukuru nyote mliochangia katika ufanisi wa kazi hii. Mwanzo kabisa namshukuru Mola kwa kunijalia kwa yote yaliyonipelekea kupata shahada hii ya uzamili ya chuo kikuu cha Nairobi.

Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa maarifa walionipa. Nawashukuru wafuatao: Prof. Habwe, Prof. Kineene, Prof. Mbatia, Dkt. Mbuthia, Prof. Iribemwangi, Dkt. Swaleh, Dkt. Zaja na Dkt. Jefwa. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Mukhwana na Dkt. Jerono. Walinipa ushauri na mwongozo ulioniwezesha kutimiza ndoto yangu.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu kwa ushirikiano waliokuwa nao katika safari hii ndefu. Wanafunzi hawa ni : Emily, Bosibori, Mutali, Kemunto, Wathe, Simion, Caro, Kimeto, Misheck na Jared.

Pia namshukuru mume wangu kwa moyo wa dhati kwa yote aliyonitendea nilipokuwa katika harakati za masomo haya.

Nyote mlioshiriki kufanikisha kazi hii nawatakia kila la heri na Mungu awabariki. Ahsanteni. Hata hivyo, endapo kuna makosa yoyote yale nabeba lawama.

## Ikisiri

Utafiti huu ulihusu athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili za Gusii Highlights na Daraja mbili mjini Kisii. Kuwepo kwa matokeo yasiyoridhisha katika somo la Kiswahili katika miaka ya hivi karibuni katika shule hizi kulihitaji utafiti ili kubaini sababu za kutokea kwa hali hii. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuchanganua makosa ya kimofolojia na kisemantiki yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule hizi. Utafiti huu ulitathmini ni kwa kiwango gani Sheng huchangia kutokea kwa makosa hayo. Ili kufikia malengo ya utafiti huu, baadhi ya wanafunzi kutoka vidato vyote vinne vya usomi katika shule hizi waliandika insha zilizosahihishwa na makosa yaliyopatikana yanayotokana na Sheng yalichanganuliwa kwa misingi ya mtazamo wa Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu. Makosa hayo yaliainishwa katika kategoria mbalimbali kisha visababishi vya makosa hayo viliweza kubainishwa. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwepo kwa makosa hayo katika vidato vyote japo kwa asilimia tofauti tofauti. Matokeo haya yalibaini kuwa kadri mwanafunzi anavyoendelea na masomo katika vidato vya juu, makosa yanayotokana na Sheng huongezeka. Sheng imechangia pakubwa kutokea kwa makosa haya. Pia utafiti huu ulibaini mikakati ya kuzuia kutokea kwa makosa haya.

## YALIYOMO

Ungamo ........................................................................................................ i.

Shukrani ........................................................................................................ iii

Ikisiri. ........................................................................................................ iv

Yaliyomo ........................................................................................................ v

Maelezo ya dhana zilizotumiwa ........................................................................ x

**SURA YA KWANZA…………………………………………………………........1**

**USULI WA UTAFITI…………………………………………………….……..1**

1.0 Utangulizi………………………………………………………………...1

1.1 Usuli wa mada ……………………………………………………………1

1.2 Tatizo la Utafiti........................................................................................ 5

1.3 Malengo ya utafiti...................................................................................... 6

1.4 Nadharia tete.............................................................................................. 6

1.5 Sababu za kuchagua mada........................................................................... 6

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti............................................................................ 7

1.7 Msingi wa kinadharia ................................................................................. 8

1.7.1 Mtazamo wa Uchanganuzi Makosa.............................................................. 8

1.7.2 Mtazamo wa Lugha Kadirifu……………………………………………….10

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada ...................................................................... 11

1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu lugha vipindi .......... 11

1.8.2 Yaliyoandikwa kuhusu Sheng. .......... 13

1.8.3 Yaliyoandikwa kuhusu athari za Sheng .......... 14

1.8.4 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu......15

1.9 Mbinu za utafiti .......... 17

1.9.1 Mbinu za kukusanya data .......... 17

1.9.2 Mbinu za kuchanganua data .......... 18

**SURA YA PILI .......... 19**

**UUNDAJI WA LEKSEMU ZA SHENG .......... 20**

2.0 Utangulizi..........20

2.1 Mbinu za uundaji wa leksemu za Sheng..........20

2.1.1 Ukopaji .......... 21

2.1.2 Ukatizaji .......... 25

2.1.3 Uambishaji .......... 26

2.1.4 Unyambulishaji .......... 28

2.1.5 Ubadilishaji silabi .......... 29

2.1.6 Onomatopia .......... 30

2.1.7 Upolisemia .......... 31

2.1.8 Ubunaji ........ 32

2.1.9 Akronimu ........ 32

2.1.10 Uhulutishaji ........ 33

2.1.11 Uambatishaji ........ 34

2.1.12 Unyumbuzi kapa ........ 35

2.1.13 Ujenzi ghairi ........ 35

2.2 Hitimisho ........ 35

**SURA YA TATU ........ 37**

**MAHUSIANO YA FAHIWA KATIKA SHENG ........ 37**

3.0 Utangulizi ........ 37

3.1 Haiponimia ........ 38

3.2 Sinonimia ........ 39

3.3 Homonimia ........ 40

3.4 Homografu ........ 41

3.4.1 Homofoni ........ 41

3.4.2 Heterofoni ........ 41

3.5 Kapitonimu ........ 41

3.6 Polisemia ........ 42

3.7 Antonimia ........................................ 43

3.8 Hitimisho ........................................ 44

**SURA YA NNE……………………………………………………………44**

**MAKOSA KATIKA KAZI ZA WANAFUNZI………………………………………45**

4.0 Utangulizi ........................................ 45

4.1 Makosa ya kimofolojia ........................................ **45**

4.1.1 Ukopaji ........................................ 46

4.1.2 Ubunaji ........................................ 46

4.1.3 Uambishaji ........................................ 47

4.1.4 Upolisemia ........................................ 47

4.2 Makosa ya Kisemantiki ........................................ 49

4.3 Mikakati ya Kuzuia Makosa Yanayotokana na Sheng……………………………..52

4.4 Hitimisho ........................................ 53

**SURA YA TANO…………………………………………………………….54**

**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**……………………………**55**

**5.**0 Muhtasari ........................................ 55

**5**.1 Mahitimisho……………………………………………………………….56

5.2 Mapendekezo…………………………………………………………………..58

**MAREJELEO……………………………………………………………………..58**

Kiambatisho A **(**Hojaji**)………………………………………….................................**xi

Kiambatisho B (Vielelezo vya insha**)……………………….........................................**xv

## Maelezo ya dhana zilizotumiwa

Msimbo -Namna ambavyo kundi fulani la watu huwasiliana kwa kutumia miundo fulani ya maneno,nambari na ishara zinazowakilisha ujumbe fulani.

Lugha ya kwanza -Lugha ambayo mtoto hujifunza mara ya kwanza kabisa kabla ya lugha nyingine yoyote.

Lugha ya pili - Lugha ambayo mtu hujifunza baada ya lugha ya kwanza.

Uchanganuzi Makosa -Mbinu itumiwayo kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha anayojifunza mwanafunzi.

# SURA YA KWANZA

# USULI WA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inatoa habari za kimsingi kuhusu utafiti huu zikiwemo usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka yautafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

## 1.1 Usuli wa mada

Utafiti huu ulihusu athari za Sheng katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika Shule za upili mjini Kisii. Lugha ni nyenzo muhimu katika uendelezaji wa maarifa hasa katika muktadha wa shule. Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha zinazotumiwa katika kuendeleza maarifa hayo. Kiswahili nikati ya lugha zenye asili ya Kibantu kama vile Kikikuyu, Kiluhya na Ekegusii. Lugha ya Kiswahili hutumika katika shughuli za kimataifa kama vile biashara na mawasiliano katika mataifa ya Afrika Mashariki, Afrika ya Kati na Afrika Kusini. Vyuo vingi duniani hufunza lugha ya Kiswahili kama vile Chuo kikuu cha Berlin, Chuo kikuu cha Osaka na Chuo kikuu cha Moscow. Lugha ya Kiswahili hutumiwa na baadhi ya vituo vya utangazaji kama vile kituo cha utangazaji cha Uingereza (BBC), kituo cha utangazaji cha Marekani (VOA) na Redio China na katika matangazo yao. Nchini Kenya, Kiswahili ni lugha rasmi na ni somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Pia hufanywa kama mojawapo ya kozi katika vyuo vikuu. Kwa kuzingatia majukumu hayo yote, ni wazi kwamba Kiswahili ni lugha muhimu sana ikilinganishwa na lugha zingine za Kibantu. Licha ya majukumu na umuhimu huo wote, lugha ya Kiswahili inakabiliwa na changamoto kubwa ambayo ni athari za Sheng. Sheng ni lugha kipindi ya lugha ya Kiswahili iliyofanana kimuundo na lugha ya Kiswahili ila huwa na maneno mengi yaliyokopwa kutoka lugha zingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Kikikuyu. Ni kwa misingi hii ambapo katika utafiti huu tutachunguza athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika baadhi ya shule za upili mjini Kisii. Tumejikita katika shule za upili mjini Kisii kwa sababu shule za upili huhusisha

vijana ambao kwa kiasi kikubwa huhusishwa na matumizi ya Sheng katika mawasiliano yao. Wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti anuwai kuhusu maana ya Sheng, kuzuka na kuenea kwake.

Ogechi (2002) na Shitemi (2001) wanasema kuwa Sheng ni msimbo wa kijamii unaotumiwa hasa na vijana wa mijini na mashambani nchini Kenya. Maoni haya yanafungamanisha Sheng na kundi mahsusi la vijana lakini katika hali halisi, watoto na wazee nao hawajaachwa nyuma kwani wanatumia Sheng hasa katika muktadha wa nyumbani.

Mkangi (1984) naye anasema kuwa Sheng ni lugha mseto au lugha "kiunzi" ya kizazi kipya cha vijana wa mijini na mashambani nchini Kenya. Anaongezea kuwa muundo wa kisarufi wa Sheng hufanana na wa Kiswahili na lugha nyinginezo za kibantu ila hutumia maneno mengi mapya ya kubuniwa na ya mkopo kutoka lugha mbalimbali kama vile Kiingereza, Kikikuyu na Kijaluo. Nakubaliana na maoni haya kwani kutokana na utafiti wetu tuliweza kubaini kuwa Sheng hukopa maneno kutoka lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha za kiasili za Kenya.

Mukhebi (1986) naye anasema kuwa Sheng ni tukio la kitamaduni ambalo linafungamana sana na mawazo au fikra, hisia na matakwa ya watumiaji wake. Osinde (1986), Abdulaziz na Osinde (1997), Mazrui (1995) na Iribemwangi na Mukhwana (2011) nao wanakumbatia maoni haya na kuongezea kuwa Sheng ni lugha kipindi ya lugha ya Kiswahili inayohusishwa sana na vijana. Nakubaliana na maoni ya waandishi hawa kuwa Sheng ni lugha kipindi ya Kiswahili. Lugha kipindi ni lugha iliyo na msamiati unaojikita katika msimu fulani na hutoweka pindi tu msimu huu unapotamatika. Pia lugha kipindi huwa na mbinu za kiusemi zinazowatambulisha na kuwaunganisha wazungumzaji wake. Sheng imeakisi sifa hizi kwani huwa na msamiati unaobadilikabadilika jinsi wakati unavyosonga, vilevile inawaunganisha wazungumzaji kwa kujihisi kuwa ni wa kikundi kimoja, Lave na Wenger (1991). Maelezo ya waaandishi hawa wote yanakubaliana kuwa Sheng ni lugha kipindi ya Kiswahili

inayotumiwa hasa na kundi mahsusi la vijana nchini Kenya. Kundi hili huwakilisha hali ya upanuzi wa msamiati na utamaduni wa Kenya.

Chimbuko na asili ya Sheng imeelezewa na wataalamu mbalimbali. Abdulaziz na Osinde(1997) wameibuka na nadharia tete kuwa Sheng iliibuka katika mitaa ya Mashariki jijini Nairobi mnamo miaka ya sabini. Waandishi hawa wanaongezea kuwa kufuatia kupatikana kwa uhuru mwaka wa 1963, idadi ya wakazi wa Nairobi iliongezeka kwa kasi kutokana na kuhama kwa watu kutoka sehemu za mashambani hadi mjini kwa lengo la kutafuta kazi viwandani. Ingawa wafanyikazi hawa walilazimika kutumia Kiswahili katika shughuli zao za mawasiliano, walikichukia kwa sababu kilidunishwa na sera za lugha za kikoloni. Watoto wa wafanyakazi hao walilazimika kuishi katika jamii ya utatulugha, yaani lugha za kienyeji, Kiswahili na Kiingereza. Ili kuepuka matatizo ya kimawasiliano, vijana hao walibuni namna ya mawasiliano iliyofuata sarufi ya Kiswahili. Namna hii ya mawasiliano ndiyo ilitokea na kuwa Sheng hapo baadaye. Mazrui (1995) na Mpande (1990) nao wanasema kuwa Sheng ilianza mnamo miaka ya thelathini.

Spypoulos (1987) anasema kuwa Sheng ilianza miaka ya hamsini na kutia fora katika miaka ya sabini. Sababu kuu iliyomfanya kudai hivi ni kwamba, majarida na magazeti yaliyohusu Sheng yalianza kuonekana miaka ya sabini.

Webb na Kembo-Sure nao wanasema kuwa wingilugha nchini Kenya kulisababisha kuzuka kwa lugha zingine kama Sheng. Wingilugha ni hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika shughuli za kimawasiliano.

Kobia (2006) anaongezea kuwa katika miaka hii ya sabini, wazungumzaji wa Sheng waliunda baadhi ya maneno kutoka nyuma kuelekea mbele badala ya muundo wakawaida wa neno, yaani kutoka mbele kuelekea nyuma. Mbinu hii ya uundaji wa maneno ya Sheng inatumika hadi sasa na inadhihirika katika mifano ya maneno ifuatayo: manya(nyama), shoke(kesho) na risto(stori). Mifano hii inaonyesha kuwa silabi za neno

hupanguliwa na kupangwa upya huku zikipewa muundo wa kinyumenyume. Katika hali ya kawaida neno huwa na muundo wa kutoka mbele kuelekea nyuma badala ya kutoka nyuma kuelekea mbele. Kulingana na mwandishi huyu haya yote yalifanywa kwa lengo la kuwasiliana kwa lugha ambayo watu wengi hawangeweza kuifahamu.

Githiora (2002) anasema kuwa Sheng ilizuka kutoka maeneo tofauti ya makazi katika mitaa ya Mashariki mwa jiji la Nairobi kama vile Kaloleni, Bahati na Jericho. Sheng imeenea kila mahali, lakini sana ni jijini Nairobi katika mitaa ya Githurai, Kangemi, Kawangware hata Uthiru.

Mbaabu na Nzunga (2003) nao wanaongezea kuwa kufikia miaka ya sabini Sheng ilikuwa imeenea sio tu Nairobi bali pia miji mingine nchini Kenya. Madai ya waandishi hawa wote kuhusu asili na chimbuko la Sheng yanatofautia na na ndiyo sababu inayompelekea (Ngesa 2012) kusema kuwa hakuna asili moja ya Sheng.

Licha ya tofauti za maoni ya wataalamu hawa, wengi wanaelekea kukubaliana kuwa Sheng ilizuka katikati ya miaka ya sitini na sabini katika sehemu za Mashariki mwa jiji la Nairobi, kama vile Kaloleni, Mbotela, Kimathi na Jericho na imeenea katika sehemu zingine nchini Kenya.

Sheng imeanza kuashiria uhalisia mkubwa wa maisha ya kisasa katika jamii ya wakenya. Kwa mfano wasanii wengi wa muziki hutumia Sheng kuwasilisha maudhui kwa walengwa wao kupitia kwa nyimbo mbalimbali. Wasanii hawa hufanya hivi kwa sababu hii ndiyo lugha inayowavutia watu wengi wa hali na matabaka yote.Wanamuziki hawa ni kama vile Nonini na Juliani. Isitoshe vipindi vingi kwenye Runinga kama vile kipindi cha Machachari cha Citizen kimesheheni matumizi ya Sheng. Lugha kipindi hii imeenea sana nchini Kenya kiasi cha kwamba hata baadhi ya waandishi wa vitabu wanaitumia katika maandishi yao (Mbaabu 2003 na Fee na Moga 1997).

Licha ya ufanisi huu wote, matumizi ya Sheng yamelaumiwa na baadhi ya wataalamu kuwa ni sababu mojawapo kuu ya kudorora kwa viwango vya ujuzi wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Lugha hii imelaumiwa kwamba ina athari zinazosababisha wanafunzi kutozingatia mafunzo ya kanuni za kisarufi na tahajia ya Kiswahili sanifu hivyo kusababisha matokeo duni katika mitihani ya Kiswahili. Wataalamu hawa ni kama vile Momanyi (2009), Kachipela (2014), Okoto (2015) na Ndiku (2014). Madai ya waandishi hawa yanaungwa mkono na washikadau na walimu wa lugha ya Kiswahili kama vile aliyekuwa waziri wa elimu marehemu Mutula Kilonzo alipokuwa akitangaza matokeo ya kitaifa ya shule za upili Kenya (K.C.S.E) mwaka wa 2012. Waziri huyu alisema kuwa Sheng ndio chanzo kuu cha matokeo duni katika somo la Kiswahili. Madai haya yote yanatupa ari ya kuchunguza athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii. Hii ndio maana utafiti huu unafanywa ili kubaini athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Kazi za Kiswahili zilizoandikwa nawanafunzi wa shule za upili huwa na makosa mbalimbali. Makosa haya husababisha matokeo yasiyoridhisha katika mitihani ya somo la Kiswahili. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza na kutathmini iwapo Sheng husababisha makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi katika shule za upili za Gusii Highlights na Daraja mbili zilizoko mjini Kisii. Tulichunguza makosa yaliyodhihirika katika miundo ya maneno isiyokubalika kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Vilevile matumizi ya maneno na misemo isiyo ya Kiswahili sanifu inayotokana na Sheng. Maneno haya husababisha utata wa kimaana katika lugha ya Kiswahili hivyo kupotosha mawasiliano sahihi. Hali hii husababisha matokeo duni katika somo la Kiswahili. Suala la athari za Sheng kwa lugha ya Kiswahili limewahi kushughulikiwa na wataalamu wengi lakini katika udurusu wetu hatukupata utafiti wowote ulioshughulikia athari za Sheng katika shule za upili hasa katika miji midogo kama vile mji wa Kisii, ikizingatiwa kwamba Sheng imeweza kuenea sio tu Nairobi bali pia miji mingine nchini Kenya Mbaabu na Nzunga (2003). Tafiti nyingi zilizofanywa zimeegemea miji mikubwa mikubwa nchini kama vile Nairobi, Mombasa hata Nakuru.

Hali hii ilitupa mshawasha wa kutafiti kuhusu athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za upili mjini Kisii. Ili kuziba pengo hili utafiti huu umejikita katika nadharia ya Uchaganuzi Makosa na Lugha Kadirifu kuchunguza na kutathmini makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Makosa haya ni yale yanayotokana na Sheng.

### 1.3 Malengo ya utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kama yafuatayo:

i. Kuchunguza iwapo Sheng husababisha makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.
ii. Kuchunguza iwapo wanafunzi wa vidato vyote vinne vya shule za upili huathirika kwa namna sawa kutokana na Sheng.
iii. Kuchunguza iwapo nadharia ya uchanganuzi makosa inafaa katika kutathmini makosa yanayotokana na Sheng katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.

### 1.4 Nadharia tete

Utafiti huu ulielekezwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Sheng husababisha makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.
ii. Wanafunzi walio katika vidato vya juu katika shule za upili huathirika zaidi kutokana na Sheng kuliko wale walio katika vidato vya chini.
iii. Nadharia ya uchanganuzi makosa inafaa katika kutathmini makosa yanayotokana na Sheng katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.

### 1.5 Sababu za kuchagua mada

Sheng ni lugha kipindi ya Kiswahili inayokua na kuenea kwa kasi sana na hutumiwa na vijana kama kitambulisho cha ujana wao, Habwe na Karanja (2004). Ni bayana kuwa jinsi lugha hii inavyokua na kuenea kwa kasi, ndivyo athari zake kwa lugha ya Kiswahili zinavyoenea. Ni kwa sababu hii tuliamua kutathmini athari za Sheng katika utendaji wa

wanafunzi ambao ni vijana katika somo la Kiswahili mjini Kisii. Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa Sheng imekuwa njia ya mawasilianokatika jamii naimeenea katika miji mingi nchini Kenya, Githiora (2002) na Mbaabu na Nzunga (2003). Kutokana na hali hii, pana haja ya kuchunguza athari za Sheng kwa lugha ya Kiswahili katika miji midogo midogo nchini Kenya kama vile mji wa Kisii.

Tetesi kutoka kwa baadhi ya wataalamu kuwa Sheng husababisha kudorora kwa lugha ya Kiswahili kama vile Momanyi (2009) na Okoto (2015) zilitufanya kujaribu kubaini ukweli wa madai haya katika sehemu tofauti tofauti nchini Kenya kama vile maeneo ya Kisii.

Utafiti huu utawafaa walimu wanaofunza somo la Kiswahili katika maeneo ya Kisii kwani wataweza kubaini athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika maeneo hayo. Walimu hawa wataweza kubuni mbinu mwafaka za kukabiliana na changamoto hii, ikizingatiwa kuwa leksemu za Sheng hutofautiana kulingana na maeneo ambapo lugha kipindi hii huzungumzwa, Githinji (2006). Hivyo leksemu za Sheng zinazotumiwa na wanafunzi katika shule zilizoko mjini Kisii huenda zikawa ndizo hutumika katika maeneo mengine ya Kisii. Hali ya kutokea kwa matokeo yasiyoridhisha katika somo la Kiswahili katika shule hizi kunatufanya kubaini iwapo Sheng huchangia kutokea kwa hali hii. Sababu ya kuchagua mji wa Kisii ni kuwa mji wa Kisii ndio mji mkuu wa eneo lote la Kisii, hivyo watu kutoka sehemu mbalimbali za Kisii hujumuika pale kwa shughuli mbalimbali ikiwemo elimu. Hivyo pana uwezekano wa matokeo ya utafiti huu kudhihirika katika shule zingine za maeneo haya.

Tumechagua kushughulikia shule za upili kwa kuwa ni kiwango muhimu katika mfumo wa 8-4-4 nchini Kenya kinachounganisha shule za msingi na vyuo.

**1.6 Upeo na mipaka ya utafiti.**

Katika utafiti huu tulitathmini athari hasi zinazosababishwa na Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule mbili za upili mjini Kisii. Shule hizi ni Shule ya upili ya Daraja Mbili na shule ya upili ya Gusii Highlights. Ili kupata athari hizi tulichunguza makosa yaliyojitokeza katika insha za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule

hizi. Tulijikita hasa katika viwango viwili vya sarufi ambavyo ni viwango vya mofolojia na semantiki. Utafiti huu ulichunguza iwapo athari hizi hujitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa viwango vyote vya shule za upili; kidato cha kwanza hadi kidato cha nne na kwa kiasi gani.

Tulichunguza makosa katika miundo ya maneno isiyofaa iliyotumiwa katika insha za Kiswahili. Pia tulichunguza jinsi maana mbalimbali za maneno ya Sheng husababisha utata wa kimaana yanapotumika katika lugha ya Kiswahili hivyo kupotosha maana inayokusudiwa. Tulizingatia matumizi yasiyofaa ya mofimu mbalimbali kama vile mofimu za umoja na wingi, mofimu za hali ya ukubwa na udogo vile vile viambishi awali na tamati katika maneno ya Kiswahili yanayotokana na Sheng.

## 1.7 Msingi wa kinadharia

Makosa katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi huelezewa katika mitazamo mbalimbali ikiwemo Uchanganuzi Linganuzi, Uchanguzi Makosa na Lugha Kadirifu. Katika utafiti huu tuliongozwa na mtazamo wa Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu.

### 1.7.1 Mtazamo wa Uchanganuzi Makosa

Mtazamo wa Uchanganuzi Makosa uliasisiwa na Corder na wenzake katika miaka ya 1960. Mtazamo huu uliibuka ili kukidhi upungufu wa mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi uliokuwa unatumiwa na baadhi ya wanaisimu kukisia makosa yanayosababishwa na lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Upungufu huo ni kama kupuuza na kutozingatia makosa ambayo hayatokani na lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Pia mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi haungeweza kutabiri makosa yaliyotokana na visababishi vingine isipokuwa yale yanayotokana na lugha ya kwanza. Uchanganuzi Makosa hutumiwa kuthibitisha makosa yote yanayopatikana katika lugha ya mwanafunzi. Uchanganuzi Makosa huchunguza aina ya makosa, visababishi vyake na namna ya kutathmini na kukabiliana na makosa hayo.

Larsen (1992) naye ameongezea kuwa mtazamo wa Uchanganuzi Makosa huchunguza idadi ya makosa ya wanafunzi wanapojifunza lugha. Mtazamo huu ulitufaa katika utafiti huu kwani utafiti wenyewe ulihusu kuchunguza na kutathmini makosa ya kimofolojia na

kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii yanayotokana na Sheng. Mtazamo wa Uchanganuzi Makosa ulitufaa katika kuchunguza utendaji wa wanafunzi katika uandishi wa insha. Corder amependekeza hatua zifuatazo katika kuchanganua makosa:

i. Kukusanya data/ sampuli kutoka kwa kazi zilizoandikwa.
ii. Kutambua makosa.
iii. Kuyaainisha makosa.
iv. Kueleza chanzo cha makosa hayo.
v. Kusahihisha na kerekebisha makosa hayo.

Kwa mujibu wa yaliyomo katika mtazamo huu, kazi zilizoandikwa na wanafunzi hukusanywa, makosa hutambuliwa na kupigiwa msitari. Makosa haya huainishwa na kuwekwa katika makundi mbalimbali kama vile makosa ya kifonolojia, ya kimofolojia, ya kisintaksia na ya kisemantiki. Makosa haya hutafutiwa visababishi vyake kama vile ujumlishaji mno, tafsiri ya moja kwa moja, hata ukosefu wa utaratibu mmoja wa kuendeleza maneno. Makosa haya husahihishwa na kurekebishwa kwa kuonyesha majibu yaliyostahili kwenye karatasi ya mwanafunzi. Kwa kufanya hivi mwanafunzi anapoipitia kazi iliyosahihishwa na kuona makosa aliyoyafanya na majibu yaliyostahili, atayaepuka makosa hayo katika kazi zitakazofuata. Isitoshe mwalimu anapoidurusu kazi hiyo darasani, ataweza kumwelezea mwanafunzi visababishi vya makosa yale hivyo mambo haya yatasaidia kurekebisha makosa hayo.

### 1.7.2 Mtazamo wa Lugha Kadirifu

Mtazamo wa Lugha Kadirifu uliasisiwa na Selinker katika mwaka wa 1969. Selinker (1969) anasema kuwa Lugha Kadirifu ni lugha inayoundwa na wanaojifunza lugha ya pili na huwa kati ya lugha ya kwanza na lugha lengwa. Lugha hii huundwa kutokana na hali ya kutoimudu lugha lengwa kikamilifu. Lugha Kadirifu imekuwa kiini cha ukuaji wa lugha ya pili.

Selinker (1969) ameeleza mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika kuchanganua makosa katika matumizi ya lugha. Mifanyiko hii ni pamoja na:

i. Uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza.
ii. Ujumlishaji mno wakanuni za lugha lengwa
iii. Uhamishaji wa ufundishaji
iv. Mikakati ya mawasiliano katika lugha ya pili
v. Mbinu za kujifunza

Uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza huhusisha matumizi ya sheria za lugha ya kwanza katika lugha lengwa. Kwa mfano baadhi ya lugha za kwanza hutumia mofimu ya udogo {ka}, ilhali mofimu ya udogo katika Kiswahili ni {ki}. Uhamishaji huu unaweza kutokea katika lugha ya kwanza, pili na tatu. Uhamishaji kama huu unapofanywa huzua makosa katika miundo ya maneno husika. Ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa hutokea pale ambapo mwanafunzi hutumia kanuni fulani katika vipengele vingi kinyume na sheria za lugha ya pili. Kwa mfano matumizi ya vivumishi vya idadi: wawili, watatu, wanne, watano, *wasita na *wasaba.Uhamishaji wa ufundishaji huhusu kutumia yale ambayo yamesomwa kutoka vitabuni au walimu wanaofunza lugha husika. Wanafunzi huiga waliyoyasoma vitabuni endapo yana makosa, makosa hayo hujitokeza katika kazi za wanafunzi hawa. Hali hii pia hujitokeza wanafunzi wanapoiga yale yanayozungumzwa na walimu wao. Endapo walimu hawa hutumia lugha iliyo na makosa, ni dhahiri kuwa wanafunzi watatumia lugha ileile katika kazi zao hivyo kufanya makosa. Mbinu za kujifunza huhusu mbinu ambazo mwanafunzi hubuni ili kumwezesha kuelewa baadhi ya vipengele katika lugha ya pili. Mbinu hizi ni kama vile kukariri kile ambacho amekisoma. Mikakati ya mawasiliano katika lugha ya pili huhusisha mbinu anazozitumia mwanafunzi ili kurahisisha mawasiliano katika lugha lengwa. Mbinu hizi mara nyingi hukiuka kanuni za lugha husika. Kwa mfano kubadilisha muundo wa neno fulani lililo gumu kutamkika katika lugha lengwa ili litamkike kwa urahisi. Matumizi ya mbinu hizi husababisha makosa katika lugha ya pili.

Mifanyiko hii ilitufaa katika kuchanganua baadhi ya makosa katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi. Hivyo mitazamo ya Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu ndiyo tuliyotumia kutathmini athari za Sheng kwa lugha ya Kiswahili kama zilivyojitokeza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.

## 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Wataalamu wengi wamefanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha vipindi na athari zao kwa lugha zingine. Hata hivyo ari yetu ya kuchunguza athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii ni kuwa kati ya kazi hizi zote zilizoandikwa, hakuna ile iliyozungumzia athari za Sheng kwa wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii katika viwango vya mofolojia na semantiki. Hata hivyo tumeyatilia maanani yote yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti.

### 1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu lugha vipindi

Lugha vipindi ni lugha zilizo na maneno na misemo iliyojikita katika kipindi fulani cha wakati na hutoweka pindi tu kipindi hiki kinapoisha (Iribemwangi na Mukhwana 2011). Waandishi hawa wanaongezea kuwa lugha vipindi huwa na mbinu za kiusemi zinazowatambulisha wazungumzaji wake. Ninayaunga mkono maoni ya wataalamu hawa kwani lugha vipindi nyingi huwa na visawe vingi na vingine huachwa kutumiwa na vingine vipya kubuniwa jinsi wakati unavyozidi kusonga.

Githiora (2002) anasema kuwa lugha kipindi ya Swanglish huzungumzwa nchini Tanzania. Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha rasmi nchini humo. Swanglish ni lugha kipindi ya lugha ya Kiswahili na inahusisha lugha za kienyeji na Kiswahili. Vijana huitumia lugha hii sana katika muziki, video hata miundo mipya ya mavazi. Mwandishi huyu anaendelea kusema kuwa Swanglish imeanza kutumiwa na vijana hata katika muktadha wa darasani hivyo kuathiri lugha ya Kiswahili. Mifano ya maneno ya Swanglish ni kama ifuatayo: mzuka (vizuri zaidi) na bomba (sawasawa). Katika mifano hii ni dhahiri kwamba maneno hupewa maana tofauti ili kuakisi mfumo wa lugha kipindi hii. Mfano neno “bomba” katika Kiswahili sanifu lina maana ya kifaa chenye shimo katikati cha kupitisha maji au moshi. Neno hili limepewa maana tofauti katika Swanglish kwa maana ya sawasawa.

Sabiti (2015) ameangazia lugha kipindi ya Uglish nchini Uganda. Lugha ya Kiingereza ndiyo lugha rasmi nchini humo. Uglish ni lugha kipindi ya Kiingereza nchini Uganda. Uglish hupata maneno yake kutoka lugha za Luganda, lahaja zingine na Kiingereza. Kuzuka na kuenea kwa Uglish kila uchao, kunashusha viwango vya elimu nchini humo.

Mifano ya maneno ya Uglish ni kama vile: dirten (chafua) na cowardice (woga). Kutokana na mifano hii tunabaini kuwa lugha ya Kiingereza inayotumiwa katika Uglish si sanifu. Mfano neno "dirten" katika Kiingereza sanifu linafaa kuwa "make dirty". Vilevile neno "cowardising" katika Kiingereza sanifu linafaa kuwa "like a coward".

Nguemo (2008) ameangazia lugha kipindi ya Naijalingo nchini Nigeria. Naijalingo ni lugha kipindi ya Kiingereza nchini humo. Lugha ya Kiingereza ndiyo lugha rasmi nchini Nigeria. Naijalingo hupata maneno yake kutoka lugha za Yoruba, Igbo, Hausa na Kiingereza. Naijalingo hutumiwa sana na vijana kwa lengo la kufanikisha mawasiliano yao na kubana ujumbe kutoka kwa wasiohusika. Lugha kipindi hii huleta utata wa kimaana hasa inapotumika katika muktadha wa darasani. Hili hutokana na sababu kuwa maneno yenye asili ya Kiingereza hupoteza maana zao za asili kila yanapotumiwa katika Naijalingo.Vilevile misamiati ya Naijalingo hujitokeza katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi hivyo kuleta utata wa kimaana. Mifano ya maneno ya Naijalingo ni kama ifuatayo: 'how body' (habari yako) na 'no long thing' (hakuna matata). Katika mifano hii maneno katika lugha ya kiingereza yametumiwa kwa maana tofauti na maana asilia. Kwa mfano maneno "how body" kwa maana ya habari yako katika Uglish yana maana tofauti katika Kiingereza sanifu.

Branford (1980) ameshughulikia lugha vipindi za Afrikaanerisms nchini Afrika Kusini. Lugha ya Kiingereza ndiyo lugha rasmi nchini Afrika kusini. Afrikaanerisms ni lugha vipindi za lugha ya Kiingereza nchini humo. Lugha vipindi hizi huhusisha lugha ya Afrikaans, lugha zingine za kiafrika na lugha ya Kiingereza. Wazungumzaji wa Afrikaans ni waafrika wanaotumia lugha hii kama lugha ya kwanza na Kiingereza kama lugha ya pili. Mifano ya Afrikaanerisms ni kama ifuatayo: antie (mwanamke mwenye mamlaka fulani) na anties (maziwa ya mwanamke).

Amanda (2011) ameangazia lugha kipindi ya Namlish nchini Namibia. Kiingereza ndiyo lugha rasmi nchini humo. Namlish ni lugha kipindi ya Kiingereza nchini Namibia. Namlish hutumiwa sana na vijana katika mawasiliano yao. Mwandishi huyu anaongezea kuwa lugha hii huathiri utendaji wa vijana hawa kila wanapohitijika kutumia Kiingereza sanifu. Namlish hupata maneno yake kutoka kwa lugha za Oshiwambo, Karango, Darama

na Herero. Mifano ya maneno katika Namlish ni kama yafuatayo: washup?(nini cha mno?) na is it?(kweli?). Ni bayana kuwa Kiingereza kinachotumiwa katika Namlish si sanifu. Mfano neno *washup* katika Kiingereza sanifu linafaa kuwa *what's up*? Kwa maana ya ni nini cha mno.

**1.8.2 Yaliyoandikwa kuhusu Sheng**

Ndiku, Mwita na Ocharo (2014) wanayaunga madai ya Muaka (2011) kuwa wanajamii wana mielekeo tofauti kuhusu Sheng. Wanaoitumia Sheng wana mielekeo chanya kuhusu matumizi yake hivyo wanatetea matumizi yake, ilhali wasiotumia Sheng wana mielekeo hasi kuihusu hivyo kulaumu matumizi yake. Tafiti hizi ni tofauti na utafiti huu kwani wanashughulikia mielekeo ya jamii kuhusu Sheng ilhali utafiti huu unashughulikia athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanasema kuwa Sheng ina msamiati mpanuzi kutokana na kubadilikabadilika kwake. Kwa mfano maneno kama manzi, chic, demu hutumiwa kwa maana moja ya msichana. Wanaendelea kusema kuwa sheng inao wingi wa tasfida. Tasfida ni matumizi ya lugha ya heshima au lugha inayoficha makali. Maoni haya yana ukweli hasa tukizingatia mifano ya maneno ya Sheng ifuatayo: kuro (kahaba), juala (kondomu) na ukedi (ukimwi). Kwa kuzingatia mifano hii ni bayana kuwa maneno ya Sheng yanapunguza makali katika lugha ikilinganishwa na maneno hayo yangetumika jinsi yalivyo.Kwa mfano neno "kuro"linampa mrejelewa heshima kidogo kuliko neno kahaba. Haya yote hufanyika kwa lengo la kuhifadhi siri miongoni mwa wahusika. Kazi hii ilifaa utafiti huu kwani tuliweza kuelewa visawe katika Sheng.

Buliba na wenzake (2006) wanasema kuwa Sheng ilitokana na maingiliano baina ya vijana wa makabila mbalimbali walioishi katika sehemu kama vile Jericho, Bahati na Kaloleni. Kwao, muundo wa sheng na wa Kiswahili hufanana. Ni kutokana na kufanana kwa miundo hii ambapo vijana huchanganyikiwa wanapohitajika kutumia muundo wa Kiswahili sanifu katika kazi zao. Maoni haya yalitusaidia kuelewa asili ya Sheng.

Githinji (2006) ana maoni kwamba tofauti za kileksia kati ya wazungumzaji wa Sheng hubainisha makundi madogomadogo ya wazungumzaji hawa. Kazi hii ilikuwa muhimu kwetu kwani ilitusaidia kuelewa miundo mbalimbali za Sheng.

Ogechi (2004) naye ameangazia jinsi leksemu za Sheng huundwa na maana zinazojitokeza kutokana na leksemu hizi. Kazi hii ilifaa utafiti huu kwani tuliweza kuelewa mbinu za uundaji wa leksemu za Sheng na kuonyesha kama kweli kimofolojia zinafanana na zile za Kiswahili au la.

Mazrui (1995) anasema kuwa Sheng ni lugha kipindi inayohusishwa na vijana wanaotoka katika jamii yenye uwezo mdogo wa kiuchumi na wanaoishi katika jiji la Nairobi. Anaongezea kusema kuwa Sheng huwatenga wenye uwezo wa kiuchumi na wasio nao. Kazi hii ilitufaa katika kuelewa asili ya Sheng.

Mahu (2009) anaihusisha Sheng na makundi yenye kutenda mambo mabaya yaliyo kinyume na maadili ya jamii kama vile: wanyaganyi, wabakaji na walanguzi wa madawa ya kulevya. Madai haya ni potovu kwa sababu Sheng inao wingi wa tasfida kama tumeshaona hapo awali. Kazi hii ilitufaa katika kuelewa mitazamo na mielekeo ya wanajamii kuhusu Sheng.

Njoroge (2014) ameangazia majukumu mbalimbali ya Sheng mjini Nakuru. Pia amedhihirisha kuwa Sheng ina majukumu mbalimbali na imepewa hadhi fulani mjini humo. Majukumu haya ni kama vile kuwasilisha maudhui muhimu katika jamii kupitia kwa muziki. Kazi hii ilitufaa katika kuelewa matumizi ya Sheng katika jamii.

### 1.8.3 Yaliyoandikwa kuhusu athari za Sheng

Okoto (2015) anadai kuwa Sheng huwafanya watu waache kutumia maneno mengine ya Kiswahili wakidhani ni Sheng. Maneno haya ni kama “demu”, katika lugha ya Kiswahili kwa maana ya kitambaa kinachotumika kufungia maziwa ya mwanamke anapolima. Neno hili hupewa maana tofauti katika Sheng nayo ni msichana. Mfano mwingine ni neno ‘kuro”, katika Kiswahili lina maana ya mnyama wa porini anayefanana na kulungu lakini katika Sheng linamaanisha kahaba. Hali hii inaashiria kuwa Sheng hupotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili. Utafiti wake ni tofauti na utafiti huu kwani utafiti

wake unahusu athari za Sheng kwa Kiswahili ilhali utafiti huu unahusu athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii.

Odhiambo (2013) ameangazia utata unaozuka kwa waumini walio na umri wa juu na watoto wadogo wasioelewa Sheng katika dini za kisasa. Anasema kuwa waumini hawa hufungiwa nje hasa katika nyimbo za injili zilizosheheni lugha ya Sheng. Utafiti huu umetufaa kwani tuliweza kuoanisha maonina mielekeo ya wanajamii kuhusu athari za Sheng katika dini na elimu. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani ameangazia athari za Sheng katika dini ya Kikristo ilhali utafiti huu unaangazia athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii.

Momanyi (2009) anasema kuwa Sheng hushusha viwango vya uelewa wa Kiswahili sanifu. Anapendekeza kuwa Sheng inafaa kuachiwa wanamuziki na utingo wa magari. Ametoa mapendekezo ya tafiti zaidi kuhusu Sheng zifanywe ili kubaini maenezi na athari zake katika elimu katika maeneo tofautitofauti nchini Kenya. Kazi yake imetufaa kwani imekuwa kama msingi bora wa utafiti huu unaonuia kutafiti kuhusu athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii.

Kachipela (2014) naye ameangazia makosa mbalimbali wanafunzi wa shule za msingi hufanya katika kazi zao za Kiswahili yanayosababisha matokeo duni katika somo hilo. Utafiti wake unaonyesha kuwa Sheng huathiri utendaji wa wanafunzi katika kazi zilizoandikwa za Kiswahili. Utafiti wake ni wa upeo tofauti na wetu kwani kiwango cha elimu alicho kishughulikia ni shule za msingi ilhali utafiti huu ni wa kiwango cha shule za upili. Mapendekezo yake yametufaa kwani alipendekeza tafiti kuhusu athari za sheng katika shule za upili na vyuo zifanywe. Hivyo utafiti wake ulikuwa msingi bora wa tatizo letu la utafiti.

### 1.8.4 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu

Corder (1967) anaeleza kuwa kila lugha ina muundo wake na kuhamisha sauti au mpangilio kutoka lugha moja hadi nyingine hudhihirika kama kosa. Amependekeza hatua zinazofaa kufuatwa katika uchanganuzi makosa. Kazi yake ilitufaa kuelewa sababu za makosa katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini

Kisii. Pia hatua ambazo alizipendekeza katika kuchanganua makosa katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi, zilitufaa kutimiza malengo ya utafiti wetu.

Larsen (1992) naye anasema kuwa nadharia ya Uchanganuzi Makosa huchunguza idadi ya makosa ya wanafunzi wanapojifunza lugha. Kazi hii ilitufaa katika uchanganuzi wa makosa kwa kuyahesabu ili kupata asilimia ya makosa katika kila kidato. Hii ni sehemu muhimu katika utafiti huu.

Selinker (1969) ametoa mifanyiko mitao ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika kuchanganua matatizo katika matumizi ya lugha. Mifanyiko hii ni pamoja na: ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa, uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza, uhamishaji wa ufundishaji, mikakati ya mawasiliano katika lugha ya pili na mbinu za kujifunza. Kazi hii ilitufaa katika kuelewa baadhi ya sababu za kutokea kwa makosa.

Seliker (1972) anasema kuwa sifa kuu ya lugha kadirifu ni kwamba, kwa wakati fulani lugha hii huacha kukua na hivyo anayejifunza lugha ya pili hawezi kufikia umilisi ki-kamilifu wa lugha lengwa. Kazi hii ilituwezesha kuelewa kuwa kazi zinazohusu ujifunzaji wa lugha huwa na makosa.

Gass na Selinker (2008) wanasema kuwa kuna uwezekano wa kuchanganua vipengele vingi vya lugha kwa kutumia mtazamo wa Lugha Kadirifu kama vile: sarufi, fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki. Kazi hii ilitufaa katika kuelewa kuwa tunaweza kutumia mtazamo wa lugha kadirifu kuchanganua makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.

Kitsao (2015) naye anasema kuwa wanafunzi wa shule za msingi hufanya makosa ya kisarufi katika kazi za insha za Kiswahili. Mwandishi huyu amejikita katika kipengele cha kimofosintaksia na kisemantiki. Kazi hii ni tofauti na yetu kwani kiwango cha elimu alichokishughulikia ni tofauti na chetu, ameshughulikia kiwango cha shule za msingi ilhali utafiti huu unashughulikia kiwango cha shule za upili. Vilevile utafiti wetu unashughulikia makosa ya kimofolojia na Kisemantiki yanayosababishwa na Sheng.

Akoth (2015) anasema kuwa wanafunzi ambao lugha yao kwanza ni Kisuba, huathiriwa na lugha hii kila wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ni wa upeo tofauti na wetu kwani utafiti wetu unachunguza athari za Sheng kwa lugha ya Kiswahili zinazotokana na Sheng ilhali utafiti wake ulihusu athari za Kisuba kwa lugha ya Kiswahili.

Obara (2014) anasema kuwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Ekegusii hufanya makosa kila wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Hata hivyo kazi hii ni ya upeo tofauti na yetu. Kazi hii ilitufaa kubainisha makosa yanayotokana na Ekegusii katika lugha ya Kiswahili.

## 1.9 Mbinu za utafiti

Ili kufikia malengo ya utafiti huu tulifuata taratibu maalum. Utafiti huu ni fafanuzi kwa vile ulihusu uchunguzi wa data na kueleza jinsi ilivyo. Tuligawa mbinu za utafiti katika sehemu mbili. Sehemu hizi ni kama zifuatazo: mbinu za kukusanya data na mbinu za kuchanganua data.

### 1.9.1 Mbinu za kukusanya data

Data ya kimsingi tuliyotumia katika utafiti huu ni insha zilizoandikwa na wanafunzi wa shule mbili za upili mjini Kisii. Data ya pili tuliipata kutoka maktabani ambapo tulitalii maandishi mbalimbali ili kubaini yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia ambayo ingetufaa. Tulinuia kutekeleza uchunguzi kifani ambapo shule mbili mahsusi za Daraja Mbili na Gusii Highlights ndizo tulizotumia kupata data. Shule hizi ni kati ya shule kama vile: shule ya wasichana ya Nyanchwa, shule ya wavulana ya Nyanchwa, shule ya upili ya Kisii, shule ya wasichana ya Nyabururu, shule ya wasichana ya Kereri na shule ya mseto ya Kanunda. Shule hizi zote zimejengwa mjini Kisii, Kaunti ya Kisii. Uchaguzi wa shule hizi umechochewa na kuwepo kwa matokeo yasiyoridhisha katika somo la Kiswahili katika miaka ya hivi karibuni. Hojaji ilitumiwa kupata maoni na mielekeo ya walimu kuhusu athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili. Insha tuliyowapa wanafunzi ilikuwa ya kiubunifu. Insha za kiubunifu ni sehemu muhimu kwenye silabasi ya shule za upili nchini Kenya inayohitaji kufunzwa na pia kutahiniwa. Kielelezo cha insha yenyewe kilikuwa kama kifuatacho:

*(Kwa kutumia maneno yasiyopungua 400, kamilisha insha ifuatayo). Siku tuliyokuwa tunaisubiri kwa hamu na ghamu ilikuwa imewadia. Niliamka asubuhi na mapema…*

Tulitumia jumla ya wanafunzi mia moja na kumi na wawili, wanafunzi hamsini na sita kutoka kwa kila shule, hivyo jumla ya wanafunzi kumi na wanne kutoka kwa kila kidato kwa kila shule. Tulitumia jumla ya walimu saba, watatu kutoka shule ya Gusii Highlights na wanne kutoka shule ya Daraja mbili. Hawa wote ni walimu wa Kiswahili katika shule hizi mbili. Wanafunzi walitoka katika vidato vyote vinne na ni wa jinsia zote mbili. Ili kupata wanafunzi hawa, wanafunzi wote wa shule hizi mbili walipewa mjarabu huu kisha kwa kuongozwa na rekodi za utendaji wa wanafunzi wa kila kidato katika somo la Kiswahili, tulidondoa insha za wale wanafunzi ambao matokeo yao katika somo la Kiswahili hayaridhishi. Hawa ndio wanafunzi na walimu tuliowatumia kupata data. Tumechagua kutumia idadi ndogo ya watafitiwa kwa sababu katika utafiti wa kisayansi data kubwa haina uhakika wa kutupa matokeo tunayotaka (Mugenda na Mugenda 1999). Makosa yanayotokana na Sheng tuliyabainisha kwa kuzingatia matumizi ya maneno ya Sheng katika lugha ya Kiswahili na miundo ya Sheng inapotumiwa katika maneno ya Kiswahili. Pia maneno ya Kiswahili yanapotumiwa kwa maana ya Sheng. Makosa ya aina hii huwa tofauti na yale yanayotokana na visababishi vingine kama vile yale makosa yanayotokana na lugha ya kwanza.

### 1.9.2 Mbinu za kuchanganua data

Tulitumia mbinu za Uchanganuzi Makosa zilizopendekezwa na Corder(1967) na Lugha Kadirifu zilizopendekezwa na Selinker (1969) kuchanganua data. Baada ya kukusanya kazi zilizoandikwa na wanafunzi, tulizisahihisha na kutambua makosa. Makosa hayo yalibainishwa kwa kupigiwa msitari, kisha yakaainishwa kwa kuyaweka kwenye kategoria zao kama vile makosa ya kifonolojia, makosa ya kimofolojia, makosa ya kisintaksia na makosa ya kisemantiki. Kwa vile utafiti huu ulijikita katika makosa ya kimofolojia na kisemantiki, makosa katika viwango vingine hayakushughulikiwa. Idadi ya makosa katika kategoria hizi kwa kila kidato ilijumuishwa ili kupata idadi ya jumla kwa kila kategoria. Tulitafuta asilimia ya makosa ya kila kategoria kwa kila kidato. Vyanzo vya makosa haya vilibainishwa. Makosa hayo yalirekebishwa kwa kuonyesha

majibu sahihi kwenye karatasi ya mwanafunzi. Mbinu tulizotumia kukusanya na kuchanganua data zitasaidia kuoyesha utendaji wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Makosa yaliyojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi yanayosababishwa na Sheng, yataonyesha athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii

# SURA YA PILI

# UUNDAJI WA LEKSEMU ZA SHENG

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia mbinu mbalimbali ambazo Sheng hutumia katika kujiundia leksemu zake. Mbinu hizi za uundaji wa leksemu za Sheng ndio huwa chanzo kikuu cha athari zinazosababisha makosa katika lugha ya Kiswahili kama tutakavyoona katika sura ya nne. Makosa haya hudhihirika katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Sheng hupata leksemu zake kutoka kwa lugha mbalimbali (Osinde 1986, Abdulaziz na Osinde1997 na Ogechi 2002). Leksemu hizi zinapotolewa katika lugha yake asili na kujumuishwa katika Sheng, hupitia mabadiliko mbalimbali. Je, leksemu ni nini? Crystal (1980) anavyonukuliwa na (Mdee 2011) anafafanua maana ya leksemu kwa kusema kuwa, leksemu ni kipashio dhahania kinachowakilisha maumbo kadha yanayotokana nacho.

Kutokana na maelezo haya tunapata kuelewa kuwa leksemu ni mzizi wa neno ambapo maneno mengine huweza kuundwa kutokana nao. Kwa mfano mzizi –refu-(ndefu, mrefu, kirefu, warefu) na mzizi –baya-(mbaya, wabaya, kibaya).

Katika mifano hii –**refu** na –**baya** ni leksemu. Sababu ni kwamba kutokana na leksemu hizi tunaweza kuunda maneno mengine kama vile: ndefu, mrefu, warefu, kibaya na wabaya. Leksemu ndizo hubeba maana katika lugha. Leksemu inaweza kuwa neno lakini si kila leksemu ambayo ni neno wala si kila neno ni leksemu. Baadhi ya leksemu za Sheng hubadili maana zinapohamishwa kutoka lugha asili vilevile maana hizi hubadilika badilika, Waithira (2011). Wakati mwingine muundo asili wa leksemu hizi huweza kufanana na muundo mpya katika Sheng lakini maana zinazowakilishwa na leksemu hizi zikawa tofauti kabisa. Leksemu katika lugha yoyote huundwa kwa kutumia mbinu za kimofolojia.

Sheng nayo kama lugha zingine hutumia mbinu za kimofolojia katika uundaji wa leksemu zake. Uundaji wa leksemu ni uunganishaji wa mofimu moja au zaidi hadi kufikia kiwango cha mofimu hiyo kuleta maana kileksika katika lugha yoyote (Mweri

2010). Maelezo haya yanatupelekea kuelewa kuwa uundaji wa leksemu huhusisha mofimu mbalimbali zinazowekwa pamoja kwa kuzingatia kaida fulani katika lugha husika ili kuleta maana inayokusudiwa katika lugha hiyo.

Mbinu za kimofolojia zinazotumika katika uundaji wa leksemu katika lugha ni pamoja na: ukopaji, ukatizaji, uambishaji, unyambulishaji, ubadilishaji silabi, onomatopia, upolisemia, ubunaji, akronimu, uhulutishaji, uambatishaji, unyumbuzi kapa na ujenzi ghairi. Katika utafiti huu tulibaini kuwa mbinu kuu katika uundaji wa leksemu za Sheng ni ukopaji. Maneno mengi hukopwa kisha hupitia mabadiliko mengine isipokuwa yale yanayobuniwa. Mbinu hizi za uundaji wa leksemu katika lugha ni kama zifuatazo:

## 2.1 Mbinu za uundaji wa leksemu za Sheng

Leksemu za Sheng huundwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno kama zifuatazo:

### 2.1.1 Ukopaji

Ukopaji ni mbinu ya kuhamisha vipashio vya lugha kutoka lugha moja hadi nyingine (Mweri 2010). Vipashio vya lugha vinavyokopwa kwa kawaida huwa misamiati. Lugha inaweza kukopa msamiati kuelezea wazo jipya ambalo halikuwepo katika utamaduni wake. Lugha inayokopa huitwa lugha pokezi ilhali lugha inayokopwa huitwa lugha changizi. Ukopaji ni wa aina tatu: ukopaji si si si, ukopaji tohozi na kaleki.

#### 2.1.1.1 Ukopaji si si si

Ukopaji si si si ni pale ambapo leksemu fulani huhamishwa kutoka lugha changizi hadi lugha pokezi bila kufanyiwa mabadiliko yoyote (Habwe na Nyonje 2010). Lugha za kiafrika zimekopa kutoka lugha zingine za kiafrika. Kwa mfano lugha ya Ekegusii imekopa jina la Mungu ‘Nyasae’ kutoka kwa Wajaluo. Awali jina la Mungu kwa Wakisii ni ‘Engoro’. Kiswahili pia kimekopa baadhi ya leksemu zake kwa kutumia mbinu hii ya Ukopaji si si si. Mifano ni kama ifuatayo:

| Leksemu mkopo | Leksemu asili | Lugha changizi |
|---|---|---|
| 1. a) Jembe | Jembe | Kiingereza |
| b) Jiko | Jiko | Kiingereza |
| c) Soda | Soda | Kiingereza |
| d) Panga | Panga | Kiingereza |

Leksemu hizi za Kiswahili huwa zimekopwa moja kwa moja kutoka lugha ya Kiingereza na maana yake huwa haibadiliki. Sheng pia imeunda baadhi ya leksemu zake kwa kutumia mbinu hii ya ukopaji si si si. Mifano ni kama ifuatayo:

| Leksemu mkopo | Leksemu asili | Lugha changizi |
|---|---|---|
| 2. a) Ngiri | Ngiri | Kikikuyu |
| b) Mokoro | Mokoro | Kikikuyu |

Sawa na leksemu zilizokopwa kwa kutumia mbinu hii ya tafsiri si si si katika lugha ya Kiswahili, leksemu zilizokopwa katika Sheng huwa na maana ile ile katika lugha changizi.

**2.1.1.2 Ukopaji tohozi**

Ukopaji tohozi hutokea pale ambapo neno hukopwa kutoka lugha changizi kisha huhawilishwa ili liwe na muundo wa kimofolojia wa lugha pokezi (Iribemwangi na Mukhwana 2011). Uhawilishaji ni hali ambapo leksimu hubadilishwa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa lugha pokezi. Mathews (1997) naye anaongezea kuwa uhawilishaji hutokea pale ambapo leksemu hubadilishwa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa lugha kopa. Katika utafiti huu tulibaini mifano ya maneno ya Kiswahili yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii. Maneno haya baada ya kukopwa, hutoholewa kabla ya kuhusishwa katika lugha ya Kiswahili. Ifuatayo ni mifano ya leksemu za Kiswahili zilizoundwa kwa kutumia mbinu ya ukopaji tohozi.

| Leksemu mkopo | Leksemu asili | maana | Lugha changizi |
|---|---|---|---|
| 3. a) Televisheni | Television | Mashine ya kutazama | Kiingereza |
| b) Labda | Labud | Ama | Kiarabu |
| c) Adabu | Adab | Maadili | Kiarabu |
| d) Baiskeli | Bicycle | Chombo cha usafiri | Kiingereza |
| e) Kompyuta | Compyuter | Tarakilishi | Kiingereza |
| f) Kochi | Coach | Aina ya kiti | Kiingereza |
| g) Virusi | Virus | Viini vinavyosababisha magonjwa | Kiingereza |

Kutokana na mifano hii tunapata kuelewa kuwa lugha ya Kiswahili hupata baadhi ya leksemu zake kwa kukopa maneno kutoka lugha za Kiingereza na Kiarabu. Maneno haya baada ya kukopwa hutoholewa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa Kiswahili. Hali hii inatokana na sababu kwamba Waingereza ndio waliotawala taifa la Kenya wakati wa ukoloni hivyo baadhi ya maneno ya lugha hii yaliingizwa katika lugha ya Kiswahili. Pia kutokana na mwingiliano kati ya waarabu na waswahili wa upwa wa Mashariki mwa Kenya wakati wa enzi za ukoloni, Kiswahili kilikopa baadhi ya maneno ya Kiarabu. Leksimu mkopo na leksimu asili huwa na maana sawa. Kwa mfano neno 'labud' katika Kiarabu na neno labda katika Kiswahili yana maana moja ambayo ni ama.

Sheng nayo imekopa baadhi ya leksemu zake kutoka lugha tofauti tofauti. Mifano katika Sheng ni kama ifuatayo:

| Leksemu mkopo | Maana | Leksemu asili | Lugha changizi |
|---|---|---|---|
| 4 a) Masa | Mama | Mother | Kiingereza |
| b) Fomu | Mpango | Form | Kiingereza |
| c) Afta | Baada | After | Kiingereza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| d) Githaa | Wakati | Thaa | Kikikuyu |
| f) Mokoro | Mzee | Omokoro | Ekegusii |
| g) Mzae | Mzazi | Mzazi | Kiswahili |

Lugha ya Kiingereza imepewa jukumu la kuwaelekeza wanafunzi shuleni nchini Kenya. Sababu hii ndiyo huchangia kuwepo kwa leksemu zilizokopwa kutoka lugha hii katika Sheng. Maneno ya Kiingereza hukopwa, hutoholewa kisha hupewa maana mpya. Wakati mwingine maaana ya leksemu undwa hufanana na maana ya leksemu asili.

Jamii ya wakikuyu imeenea na kuzagaa katika kila pembe nchini Kenya hasa kutokana na sababu za kibiashara. Mji wa Kisii ni mojawapo ya miji iliyokaliwa na jamii hii. Ni kutokana na mwingiliano wa wakikuyu na wanajamii wengine ambapo leksemu za kikikuyu hudhirika katika Sheng inayozungumzwa katika maeneo haya.

Asilimia 90% ya wakazi wa mji wa Kisii ni wakisii wanaotumia lugha ya Ekegusii kama lugha yao ya kwanza. Hali hii imechangia kuwepo kwa leksemu za lugha Ekegusii katika Sheng inayozungumzwa hapa. Leksemu hizi ni kama matumizi ya neno ‘mokoro’. Katika lugha ya Ekegusii neno hili huwa ‘omokoro’ kwa maana ya mzee. Vile vile katika Sheng neno hili linatumiwa kwa maana ya mzee.

#### 2.1.1.3 Kaleki

Kaleki ni aina ya ukopaji ambapo maana ya neno au fungu la maneno hutafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Maneno hutafsiriwa pasi na kujali muktadha wa matumizi yake katika lugha changizi. Hali hii huweza kusababisha utata wa kimaana maneno hayo yanapotumika katika lugha pokezi. Hatukuweza kupata mifano ya maneno ya Sheng yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii. Labda ni kutokana na sababu kwamba Sheng hubadilishabadilisha msamiati wake hivyo tafsiri kama hizi hazitakuwa za maana.

Ifuatayo ni mifano ya maneno katika lugha ya  Kiswahili yaliyoundwa kwa kutumia Kaleki:

| **Kiingereza(Lugha Changizi)** | **Kiswahili(Lugha Pokezi)** |
|---|---|
| 5 a)  Co-wife | Mke mwenza |

| | |
|---|---|
| b) National Language | Lugha ya taifa |
| c) First Language | Lugha ya kwanza |
| d) Third World Countries | Mataifa ya tatu ilimwenguni |
| e) United Nations | Umoja wa mataifa |
| f) Sugar mummy | Mama sukari |
| g) Cocktail party | Karamu ya mkia wa jogoo |
| h) Basic needs | Mahitaji ya kimsingi |

Licha ya mbinu ya Kaleki kutumiwa na baadhi ya lugha nyingi katika uundaji wa leksemu zake, mbinu hii ina udhaifu wake kwani ukopaji huu huhusisha kutafsiri baadhi ya maneno kutoka lugha moja hadi nyingine. Tafsiri hizi huweza kusababisha utata wa kimaana maneno husika yanapotumiwa katika lugha pokezi. Kwa mfano *sugar mummy* kwa maana ya mama sukari.

### 2.1.2 Ukatizaji

Ogechi (2005) anasema kuwa ukatizaji ni mbinu ya kufupisha maneno kwa kudondosha silabi moja au zaidi. Iribemwangi na Mukhwana (2011) nao wanasema kuwa ukatizaji ni mbinu ya uundaji wa maneno inayohusu ufupishaji wa maneno au vifungu vya maneno. Neno lililokopwa huhawilishwa kisha hukatwa. Leksemu iliyofupishwa huweza kuongezewa viambishi ili iwe ya Sheng. Ukatizaji huweza kutokea mwanzoni, kati au mwishoni mwa neno.

Lugha ya Kiswahili ina maneno yaliyokatwa. Mifano ya maneno haya ni kama ifuatayo:

| | **Leksemu katwa** | **Leksemu asili** |
|---|---|---|
| 6 | a) Bw. | Bwana |
| | b)Bi. | Bibi |
| | c)Mke | Mwanamke |
| | d)Mume | Mwanamume |

Kutokana na mifano hii ni bayana kuwa maneno haya yamefanyiwa ukatizaji awali (Mke na Mume) na ukatizaji tamati (Bw. na Bi.). Maana ya maneno yaliyokatwa na leksemu asili huwa na maana ile ile moja.

Sheng pia inayo maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ya ukatizaji, hata hivyo maneno yaliyoundwa huwa yamekopwa kutoka lugha zingine na kutoholewa kisha yakakatwa. Mifano ya maneno haya ni kama ifuatayo:

| | **Leksemu katwa** | **Leksemu asili** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 7 | a) Nai | Nairobi | Jiji la Nairobi |
| | b) Ju | Juu | Kwa sababu |
| | c) Adi | Hadi | Mpaka |
| | d) Ka | Kama | Ulinganishaji |
| | e) Ata | Hata | Pia |
| | f) Io | Hiyo | Kuashiria kitu |

Mengi ya maneno yaliyokatwa hapa yanatawaliwa na ukatizaji awali na tamati. Ukatizaji kati haujadhihirika. Ukatizaji awali ni hali ambapo silabi za mwanzo hukatwa ilhali ukatizaji tamati ni ukatizaji wa silabi za mwisho. Maneno kama *Nai*, *Ju* na *Ka* yamefanyiwa ukatizaji tamati ilhali neno *Adi* limefanyiwa ukatizaji awali. Licha ya ukatizaji huu maana ya leksemu iliyokatwa na leksemu asili huwa haibadiliki.

### 2.1.3 Uambishaji

Uambishaji ni mbinu ya kuongeza viambishi kabla ya mzizi wa neno ili kuunda neno jipya, Mweri (2010). Viambishi hivi huambishwa kwenye mzizi wa neno. Obuchi na Mukhwana (2010) nao wanasema kuwa uambishaji ni uongezaji wa viambishi katika mzizi wa neno kwa lengo la kuunda neno jipya. Lugha nyingi hutumia mbinu hii kupata maneno mapya. Sheng hutumia mbinu hii baada ya kukopa na kutohoa leksemu kutoka lugha zingine. Katika utafiti wetu tuliweza kupata mifano ya maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii.

Lugha ya Kiswahili ina maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ya uambishaji. Mifano ni kama ifuatayo:

| | Uambishaji | Leksemu undwa |
|---|---|---|
| 8 | a) **M**+**ku**+lima | mkulima |
| | b)**Kiji**+meza | kijimeza |
| | c)**Ji**+meza | jimeza |
| | d**) U**+toto | utoto |
| | e) **ki**+toto | kitoto |
| | f) **ku**+lima | kulima |

Kutokana na mifano hii tunapata kwamba mofu zinazotumiwa huwakilisha dhana mbalimbali kama vile:{kiji} na {ki} ni mofu zinazowakilisha hali ya udogo, {Ji}ni mofu inayowakilisha hali ya ukubwa na {u} na {ku}huwakilisha hali ya unominishaji.

Sheng huitumia mbinu hii pia kujiundia leksemu mpya. Leksemu hizi hukopwa kutoka lugha zingine kisha hutoholewa kabla ya kuambishwa.

| | Uambishaji | Leksemu undwa | Maana |
|---|---|---|---|
| 9 | a) **Ka**+mtoi | kamtoi | mtoto mdogo |
| | b)**Ma**+vijana | mavijana | vijana wengi |
| | c)**Ma**+mboga | mamboga | mboga nyingi |
| | d) **Vi**+poa | vipoa | vizuri |
| | e) **Vi+**noma | vinoma | vibaya |
| | f) **Ma**+demu | mademu | wasichana |

Mofu zilizoambishwa huwakilisha dhana mbalimbali:{ma} huwakilisha hali ya wingi na {ka} huwakilisha hali ya udogo. Pia mifano hii inajumuisha mofu inayowakilisha vielezi,nayo ni {vi}. Neno noma lenye asili ya Kiswahili kwa maana ya pingamizi limepanuliwa kimaana katika Sheng na kupewa maana mpya ambayo ni –baya. Kiambishi awali vi- kinapoongezwa katika neno hili huwakilisha kielezi cha jinsi.

### 2.1.4 Unyambulishaji

Unyambulishaji ni mbinu ya kuongeza viambishi baada ya mzizi wa neno ili kuunda neno jipya. Maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ni yale ya mnyambuliko. Maneno haya huwa na maana tofauti na neno asili. Mbinu hii hutumiwa kuunda maneno mapya kutokana na maneno mengine ambayo tayari yako katika lugha hiyo.

Lugha ya Kiswahili hutumia mbinu hii kujiundia leksemu zake kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| | Unyambulishaji | Leksemu undwa |
|---|---|---|
| 10 | a) Lim+**iw**+**a** | Limiwa |
| | b) Piga+**an**+**a** | Pigana |
| | c) Kut+**an**+**ish**+**w**+**a** | Kutanishwa |
| | d) Som+**esh**+**a** | Somesha |
| | e) Kat+**w**+**a** | Katwa |

Katika mifano hii maneno yamenyambuliwa kwa kuongezewa viambishi tamati vinavyowakilisha kauli mbalimbali za minyambuliko. Mofu zilizoambishwa huwakilisha kauli mbalimbali za minyambuliko:{an} huwakilisha kauli ya kutendana, {ish}na{esh}huwakilisha kauli ya kutendesha na {w} na {iw} huwakilisha kauli ya kutendewa.

Sheng pia haijaachwa nyuma katika kutumia mbinu hii kujiundia leksemu zake. Haya hutendeka baada ya kukopa leksemu hizi.

| | Unyambulishaji | Leksimu undwa | Maana |
|---|---|---|---|
| 11 | a) Toke+**le**+**ze**+**a** | Tokelezea | Pendeza/onekana ghafla |
| | b) Huenda+**ga** | Huendaga | Kuenda kila mara |
| | c) Taka+**nga** | Takanga | Taka kila mara |
| | d) Oko+**le**+**a** | Okolea | Kutoa usaidizi |

Katika mifano hii maneno yamenyambuliwa kwa kuyaongezea viambishi tamati vinavyowakilisha dhana mbalimbali. Mofu zilizoambishwa katika mifano hii huwakilisha dhana kama vile {ga} na {nga} hutumika kuwakilisha hali ya mazoea. Mofu {le} huwakilisha hali ya kutendea.

### 2.1.5 Ubadilishaji silabi

Ubadilishaji silabi ni mbinu ambapo silabi za neno hupanguliwa na kupangwa upya. Neno hilo jipya hupewa muundo wa kinyumenyume, yaani neno huwa na muundo wa kutoka nyuma kuelekea mbele badala ya muundo wa kawaida wa kutoka mbele kuelekea nyuma (Ogechi 2005). Muundo wa leksemu undwa huwa tofauti na muundo wa leksemu hiyo katika lugha asilia, japo maana msingi ya neno hilo haibadiliki. Lugha ya Kiswahili imetumia mbinu hii kujiundia leksemu zake licha ya (Ngesa 2012 na Ogechi 2005) kusema kuwa mbinu hii hujitokeza katika Sheng. Mifano ya maneno ya Kiswahili yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ni kama yafuatayo:

| | **Leksemu asili** | **Leksemu undwa** |
|---|---|---|
| 12 | a) Enyi | Nyie |
| | b) Ewe | Wee |

Kutokana na mifano hii tumebaini kuwa maana ya leksemu asili na leksemu undwa hufanana.

Mifano ya maneno ya Sheng yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ni kama yafuatayo:

| | **Leksemu asili** | **Leksemu toholewa** | **Leksemu undwa** | **Lugha changizi** |
|---|---|---|---|---|
| 13 | a) Card | Kadi | Dika | Kiingereza |
| | b) Check | Cheki | Kiche | Kiingereza |
| | c) Kesho | Kesho | Shoke | Kiswahili |
| | d) Nyumba | Nyumba | Mbanyu | Kiswahili |
| | e) Story | Stori | Risto | Kiingereza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| f) Food | Fud | Dif | Kiingereza |

Maneno yaliyoundwa katika mifano hii hukopwa kutoka lugha zingine, hutoholewa kisha hupewa muundo tofauti japo maana ya leksemu asili na leksemu undwa hufanana.

### 2.1.6 Onomatopia

Onomatopia ni mbinu ambapo maneno huundwa kwa kuiga sauti/mlio wa kitu. Iribemwangi na Mukhwana(2011) wanasema kuwa maneno haya huundwa kwa kuzingatia sifa, uamilifu, umbo na sauti au mlio wa kitu. Lugha nyingi ulimwenguni hutumia mbinu hii kujiundia leksemu zao. Lugha ya Kiswahili imetumia mbinu hii kujiundia leksemu zake. Mifano ya maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ni kama ifuatayo:

| | **Leksemu undwa** | **Maana** |
|---|---|---|
| 14 | a) Tingatinga | Mashine ya kusiaga nafaka |
| | b) Kinasasauti | Kifaa cha kunasa sauti |
| | c) Patipati | Aina ya viatu vilivyo wazi juu |
| | d) Pikipiki | Chombo cha usafiri |

Maneno kama kinasa sauti yameundwa kutokana na uamilifu wa kifaa husika, maneno kama tingatinga, patipati na pikipiki yameundwa kutokana na sauti/mlio wa vifaa hivyo.

Sheng pia huunda baadhi ya maneno yake kwa kutumia mbinu hii. Mifano ya maneno yaliyoundwa ni yafuatayo:

| **Leksemu undwa** | **Maana** |
|---|---|
| 15 a) Kacha | Pingu |
| b) Mbrrrcha | Shida |
| c) Poko | Kahaba |

Sheng haijakita sana katika uundaji wa leksemu zake kwa kutumia mbinu hii ndio maana mifano yake ni michache mno kuliko lugha zingine.

### 2.1.7 Upolisemia

Upolisemia ni mbinu ya kuongeza au kupanua maana ya maneno ambayo tayari yako katika lugha (Iribemwangi na Mukhwana 2011). Maneno ambayo tayari yako katika lugha huweza kuongezewa maana ya ziada (Obuchi na Mukhwana 2010). Neno linalotumiwa katika muktadha mmoja hupanuliwa ili litumike katika muktadha mwingine. Lugha ya Kiswahili sawa na Sheng huunda maneno yake kwa kutumia mbinu hii. Ogechi (2005) naye anasema kuwa nomino kopwa katika Sheng hupata upanuzi wa maana kisemantiki. Sheng hupata maneno yake baada ya kukopa maumbo ya maneno, kisha maumbo hayo hupewa maana mpya. Mifano ya maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii katika lugha ya Kiswahili ni kama yafuatayo:

| | **Neno** | **Maana asili** | **Maana ziada** |
|---|---|---|---|
| 16 | a) Beberu | Kondoo wa kiume | Mkoloni |
| | b) Kinyonga | Mnyama aishiye kwa majani | Mtu asiye na msimamo |
| | c) Mteja | Anayeshiriki biashara | Hali ya kuzima simu |

Sheng pia ina maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii. Mifano ya maneno haya ni kama ifuatayo:

| | **Neno** | **Maana asili** | **Maana ziada** |
|---|---|---|---|
| 17 | a) Demu | Aina ya kitambaa kikuukuu | Msichana |
| | b) Mbuyu | Aina ya mti | Baba |
| | c) Poa | Kuwa baridi | Sawasawa |
| | d) Chapa | Adhibu | Kutopendeza/konda |
| | e) Dunga | Choma kwa kifaa | Vaa |
| | f) Mhadhara | Kipindi cha usomi | Shida/matatizo |

Kutokana na mifano hii tumebaini kuwa maneno hukopwakisha maana hupanuliwa kwa kupewa maana mpya iliyo tofauti na maana ya neno hilo katika lugha changizi.

### 2.1.8 Ubunaji

Mbinu ya ubunaji huchochewa na uvumbuzi wa kisayansi. Ubunifu ni mchakato wa kuunda leksemu mpya katika lugha kimakusudi kutokana na faridi za kimofolojia zilizopo (Hartman na Stork 1972). Maneno haya huundwa ili kukidhi upungufu wa kimsamiati katika lugha husika kuhusu dhana hizo mpya. Lugha nyingi huwa na sifa hii ya kubuni maneno ili kuziba pengo fulani linalohitaji kuzibwa kimsamiati.

Lugha ya Kiswahili imeunda maneno yake kwa kutumia mbinu hii. Mifano ya maneno haya nia kama ifuatayo:

| **Leksemu undwa** | **Maana** |
|---|---|
| 18 a) Tarakilishi | Kompyuta |
| b) Rununu | Simu ya mkononi |
| c) Simutamba | Simu ya mkononi |

Maneno haya hubuniwa ili kuvitajia vifaa vipya vilivyobuniwa. Sheng nayo ina maneno kadhaa iliyojiundia kwa kutumia mbinu hii. Mifano ni kama ifuatayo:

| **Leksemu undwa** | **Maana** |
|---|---|
| 19 a) Chizi | Mwenda wazimu |
| b) Nangoz | Simu |
| c) Tenje | Redio |
| d) Karao | Polisi |
| e) Orogramu | Simu |

Maneno haya ya kubuniwa hayajakopwa kutoka lugha yoyote ile bali hujitokeza tu na kupewa maana fulani. Maana hizi zinazopewa maneno haya hupatikana kutokana na uamilifu wa kitu kile au muundo wake. Kwa mfano neno *tenje* kwa maana ya *Redio*, neno hili limepewa kifaa hiki kutokana na muundo wake.

### 2.1.9 Akronimu

Akronimu ni mbinu ya kuunda maneno kwa kuchukua herufi au silabi za mwanzo za maneno hayo. Sehemu za kwanza za kila neno katika kishazi huunganishwa na kuunda

neno moja (Obuchi na Mukhwana 2010). Mbinu hii husaidia kuyafupisha maelezo ambayo kwa kawaida ni marefu. Baada ya kuunda leksemu hizi hutamkwa kama neno moja wala sio herufi tofautitofauti. Katika utafiti wetu hatukuweza kupata mifano katika Sheng labda ni kwa sababu mbinu hii huhitaji umakini fulani ili kuunda akronimu hizi ili zitumike kutimiza malengo ya kipindi kirefu cha wakati. Watumiaji wengi wa Sheng hawana umakini huo na malengo yao huwa kutimiza haja ya kimawasiliano ya kipindi kifupi.

Lugha ya Kiswahili ina akronimu kama zifuatazo:

| | **Maneno** | **Akronimu** |
|---|---|---|
| 20 | a)**Ch**ama cha **Ki**swahili Cha **Ta**ifa | CHAKITA |
| | b)**T**aasisi ya **U**chunguzi wa**Ki**swahili | TUKI |
| | c**) Ba**raza la **Ki**swahili la**Ta**ifa | BAKITA |

Akronimu hizi hutumika kimataifa wala hazibadiliki badiliki.

### 2.1.10 Uhulutishaji

Uhulutishaji ni mbinu ya kuunganisha vipashio viwili au zaidi ambavyo kwa kawaida havipaswi kuwa pamoja. Vipashio hivi huunda umbo la neno lililo na maana tofauti na maana ya maneno asili (Obuchi na Mukhwana 2010).

Lugha ya Kiswahili ina maneno iliyojiundia kwa kutumia mbinu hii.

| | **Maneno awali** | **Neno undwa** |
|---|---|---|
| 21 | a) **Ru**nunu+Ma**ninga** | -Runinga |
| | b)**M**tu+a**si**ye na+**kwao** | -Msikwao |
| | c)**Cha**kula cha **mcha**na | **-**Chamcha |

Katika utafiti huu hatukuweza kupata maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii katika Sheng labda jinsi wakati unavyozidi kusonga huenda Sheng ikaanza kuunda maneno yake kwa kutumia mbinu hii.

### 2.1.11 Uambatishaji

Fromkinna Rodman (1993) wanasema kuwa, uambatishaji ni mbinu ya kuweka pamoja maneno mawili au zaidi yaliyo huru kwa kusudi la kuunda neno lenye kusimamia dhana mpya. Neno ambatano linaloundwa huwa na maana tofauti na maneno ya awali. Lugha nyingi hujiundia maneno yake kwa kutumia mbinu hii.

Lugha ya Kiswahili  ina maneno iliyojiundia kwa kutumia mbinu hii. Mifano ya maneno haya ni  kama ifuatayo:

| | Maneno awali | Neno mwambatano |
|---|---|---|
| 22 | a) Elimu+Viumbe | Elimuviumbe |
| | b) Changa+Moto | Changamoto |
| | c) Askari+Kanzu | Askarikanzu |
| | d) Mwana+Hewa | Mwanahewa |
| | e) Komba+Mwiko | Kombamwiko |

Neno mwambatano hili lililoundwa hutamkwa kama neno moja wala sio neno moja moja. Sheng pia hujiundia baadhi ya leksemu zake kwa kutumia mbinu hii. Haya yanadhihirika katika mifano ifuatayo:

| | Maneno awali | Neno mwambatano |
|---|---|---|
| 23 | a) Oral+Gram | Orogramu(Simu) |
| | b) Chic+dame | Chikidee (Msichana) |

Maneno mawili yanayotumiwa kuunda neno mwambatano huwa na maana leksia, lakini yanapounganishwa hupoteza maana yazo asilia. Neno ambatano linaloundwa huchukua leksia iliyo tofauti na maana za maneno yaliyoliunda. Kwa mfano neno *Oral* katika lugha ya Kiingereza lina maana ya kinywani na *gram* ni kitu kilichoandikwa. Katika Sheng maneno haya hukopwa, hutoholewa, huambatanishwa kisha hupewa maana tofauti na maana asilia kwa maana ya simu.

### 2.1.12 Unyumbuzi kapa

Unyumbuzi kapa ni mbinu ya uundaji wa maneno ambapo leksemu haiwi na viambishi vya kiothografia. Katamba (1993) anasema kuwa leksemu mpya inaweza kuundwa bila ya kubadili umbo la leksemu asilia. Katika hali hii leksemu hubadilisha kategoria yake bila kuambishwa wala kufanyiwa jambo lolote linaloweza kubadili umbo la leksemu hiyo. Viambishi hivi huchukuliwa kuwa kapa.

Lugha ya Kiswahili ina maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii Mifano ni kama ifuatayo:

| | Neno asilia | Maana | Neno undwa | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 24 | a) Husudu | Wivu | Hasidi | Mwenye wivu |
| | b) Laumu | Wekea makosa | Lawama | Wekea makosa |
| | c) Taaluma | Ujuzi wa kiakademia | Taalimu | Elimu |

Maana ya neno asilia na neno undwa huwa zinakaribiana.

Katika utafiti huu hatukupata maneno ya Sheng yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii labda ni kwa sababu kwa kiasi kikubwa Sheng ni lugha ambishi na hutegemea viambishi mbalimbali ili kupata maana mbalimbali za maneno yake.

### 2.1.13 Ujenzi ghairi

Ujenzi ghairi ni mbinu ambapo leksemu hupunguzwa kimaumbo ili kuunda leksemu nyingine tofauti mara nyingi leksemu hizi huwa nomino. Leksemu inayoundwa mara nyingi huwa kitenzi (Warambo 2011). Katika utafiti huu hatukuweza kupata mifano ya maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii katika lugha ya Kiswahili na Sheng. Labda jinsi wakati unavyozidi kusonga lugha hizi zitatumia mbinu hii kujiundia leksemu zake.

## 2.2 Hitimisho

Katika sura hii tumeangazia mbinu mbalimbali za kimofolojia zinazotumiwa na Sheng katika uundaji wa leksemu zake. Tumeona kuwa muundo wa neno/ maneno kutegemea mbinu hizi za uundaji wa leksemu za Sheng hubainisha maana inayowasilishwa na neno hilo. Sheng kama lugha zingine, hutumia mbinu mbalimbali katika kujiundia leksemu zake. Mbinu hizi ni pamoja na: ukopaji, uambishaji, uambatanishaji, upolisemia,

ukatizaji, unyambulishaji, onomatopia, ubadilishaji silabi na ubunaji. Hata hivyo tuliweza kubaini kuwa mhimili mkuu katika uundaji wa leksemu za Sheng ni ukopaji. Maneno hukopwa kisha hupitia mabadiliko mengine isipokuwa yale maneno yanayotokana na ubunaji. Maneno haya hukopwa kutoka lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha zingine za kiasili.

Katika sura inayofuata tumechunguza mahusiano ya fahiwa katika Sheng. Sura hii ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa itakuwa kama mhimili wa yale tutakayoyasema katika sura ya nne ambayo itahusu uchanganuzi wa makosa.

# SURA YA TATU

# MAHUSIANO YA FAHIWA KATIKA SHENG

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia mahusiano ya fahiwa katika Sheng. Mahusiano ya fahiwa ni mojawapo ya vigezo vya kisemantiki katika lugha.Vigezo hivi husaidia katika kuelewa maana za maneno, tungo na sentensi katika lugha.Vigezo hivi ni kama vifuatavyo: kigezo cha Virai, kanuni za uzungumzaji, udondoshaji maneno, uunganishaji na kigezo cha mahusiano ya fahiwa, Mweri (2010). Kigezo cha virai husaidia kuelewa maana ya virai au sentensi katika lugha. Maana ya sentensi hutokana na uelewa wa maneno binafsi yaliyomo katika sentensi pamoja na uelewa wa kanuni za uunganishaji wa maneno hayo. Kigezo cha kanuni za uzungumzaji nacho husaidia kuelewa maana za matamko. Kigezo cha udondoshaji maneno huhusu kudondoa maneno fulani katika sentensi hasa kama maneno hayo hayana mchango wowote katika uelewa wa maana ya sentensi husika. Kigezo cha uunganishaji hushughulikia jinsi viambatishi au viunganishi huunganisha vipashio vyenye mizani sawa, ambavyo vyaweza kuwa vishazi au virai na maneno. Kigezo cha mahusiano ya fahiwa hutumika katika kupata maana ya maneno kutokana na uhusiano neno linao na maneno mengine katika lugha.

Katika hali ya kawaida maneno huwa na maana zaidi ya kile kinachoashiriwa nayo. Maana hii ya ziada ndiyo huitwa fahiwa, Mweri (2010). Obuchi na Mukhwana (2010) nao wanasema kuwa fahiwa ni maaana iliyoongezwa katika maana ya msingi ya neno na huweza kubadilika kutegemea wakati na mazingira. Maana msingi ni maana ya kwanza ya neno na haibadiliki. Kwa mfano maana za maneno mama na baba. Edmonds (2005) naye anasema kuwa fahiwa ni maana za neno moja zinazohusiana. Kutokana na maelezo ya waandishi hawa tunabaini kuwa fahiwa ni maana nyingine zinazopewa maneno ya lugha fulani kando na maana msingi. Fahiwa hizi hutumiwa na wazungumzaji wa Sheng kutungia sentensi wanazozitumia katika kufanikisha mawasiliano kati yao. Vifahiwa hivi ndivyo husababisha makosa ya kisemantiki hasa maneno ya Kiswahili yanapotumika kwa maana ya Sheng, pia maneno ya Sheng yanapotumika kwa maana ya Kiswahili. Maneno

mengi ya Sheng yana mahusiano ya fahiwa. Kwa mfano neno *Mathee* la Sheng linaweza kusaidia kueleza neno *Masa*. Sababu ni kwamba maneno haya yameundwa kwa namna sawa: yamekopwa kutoka neno la Kiingereza *Mother*, yakatoholewa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa Sheng. Pia maneno haya yana uhusiano wa usinonimia kwa kuwa maneno haya yana maana ile ile moja ya Mama. Isitoshe maneno haya huweza kuingia katika uhusiano wima kwani yanaweza kubadilishana nafasi bila kubadili maana za sentensi husika kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

*25**a**) Mathee amedoze*(Mama amelala.)

*b) Masa amedoze*(Mama amelala.)

Kutokana na mifano hii ni bayana kuwa maneno yaliyopigiwa msitari yanaweza kubadilishana nafasi bila kuathiri maana ya sentensi hizo.

Mahusiano ya fahiwa katika lugha ni kama yafuatayo: haiponimia, sinonimia, homonimia, homografu, kapitonimu, polisemia na antonimia.

### 3.1 Haiponimia

Haiponimia ni uhusiano kati ya maneno ambapo maana ya neno moja hujumuisha maana ya neno au maneno mengine, Habwe na Nyonje (2010). Briton (2000) naye anasema kuwa uhaiponimia ni uhusiano wa kiwima ambapo maana ya neno/maneno hujumuishwa katika maana ya neno jingine. Neno lenye maana pana huitwa neno jumuishi au haiponimu ilhali maneno yenye maana mahsusi huitwa haiponimia, Wamitila (2003). Lugha ya Kiswahili ina mifano ya maneno yenye uhusiano huu wa uhaiponimia.

| | Haiponimu | Haiponimia |
|---|---|---|
| 26 | a) Mnyama | Ng’ombe, mbuzi, paka, ngamia, punda |
| | b) Mtu | Mwanamme, mwanamke, mtoto |
| | c) Nguo | Sketi, kabuti, sweta, marinda |

Katika mifano hii neno mnyama ni haiponimu ilhali maneno kama vile: ng’ombe, mbuzi, paka na punda ni haiponimia.

Sheng nayo ina haiponimia zake. Mifano ni kama ifuatayo:

| Haiponimu | Haiponimia |
|---|---|
| 27 a) Waks | ukonkodi, udere, ugondi, umode |

Katika mfano huu neno *waks* lina haiponimia kama vile: u*konkodi (*utingo), u*dere (*udereva*)*, u*mode (*ualimu*)* na u*gondi (*upolisi*)*. Hali hii inaashiria kwamba maana za haiponimia hizi hujumuishwa kwenye maana ya haiponimu husika.

**3.2 Sinonimia**

Sinonimia ni uhusiano wa maumbo fulani ya maneno katika lugha kuwa na maana sawa, Habwe na Nyonje (2010). Maneno haya huweza kutumiwa katika hali ya ubadala au ubadilishanaji huru katika miktadha fulani pekee. Katika utafiti huu tulibaini mifano ifuatayo ya sinonomia katika lugha ya Kiswahili.

| | Neno | Sinonimu |
|---|---|---|
| 28 | a) Pombe | Tembo |
| | b) Mtoto | Mwana |
| | c) Maradhi | Magonjwa |
| | d) Mungu | Mola |
| | e) Binadamu | Mja |

Kutokana na mifano hii neno pombe lina maana sawa na tembo vilevile neno maradhi lina maana sawa na magonjwa.

Sheng pia ina sinonimia zake na mifano ni kama ifuatayo:

| | Neno | Sinonimu | Maana |
|---|---|---|---|
| 29 | a) Msupa | Chic | Msichana |
| | b)Doo | Ganji | Pesa |
| | c) Ndai | Dinga | Gari |
| | d) Dimbua | Sosi | Mlo |
| | e) Masa | Mathee | Mama |

Katika mifano hii maneno *doo* na *ganji* ni sinonimu. Pia maneno *Ndai* na *Dinga* ni sinonimu kwa sababu maneno haya yana maana sawa.

### 3.3 Homonimia

Homonimia ni uhusiano ambapo maneno huwa yanafanana katika maumbo yake lakini huwa na maana tofauti kimsingi, Obuchi na Mukhwana (2010). Maneno haya pia hutamkwa kwa namna sawa lakini maana zao huwa hazina uhusiano wowote. Mifano ya homonimia katika lugha ya Kiswahili ni kama ifuatayo:

| | **Neno** | **Maana** |
|---|---|---|
| 30 | a) Panda | Weka mbegu mchangani |
| | b) Panda | Elekea sehemu iliyo juu |
| 31. | a) Ua | Toa uhai |
| | b) Ua | Sehemu ya mmea iliyochanua |

Katika mifano hii neno panda katika mfano 30(a) na panda katika 30(b) ni homonimia kwa kuwa yanafanana kimuundo, hutamkwa kwa namna sawa lakini maana zao ni tofauti. Pia hali hii inajitokeza katika mfano 31(a) na31( b) kwenye neno ua.

Sheng nayo ina maneno yenye mahusiano ya kihomonimia. Mifano ni kama ifuatayo:

| | **Neno** | **Maana** |
|---|---|---|
| 32 | a) Chapa | Filisika |
| | b) Chapa | Konda |
| | c) Chapa | Zeeka |
| 33 | a) Keja | Nyumba ya mtu |
| | b) Keja | Nyumba ya mbwa |
| | c) Keja | Nyumba ya kuku |

Katika mifano hii neno *chapa* katika mfano 32(a) na *Chapa* katika 32(b) na *Chapa* katika 32(c) ni homonimia kwa sababu hutamkwa kwa namna sawa, miundo yao inafanana lakini maana zao ni tofauti. Hali hii vilevile hujitokeza katika mfano 33 a, b na c.

### 3.4 Homografu

Homografu ni uhusiano wa maneno yaliyo na maumbo sawa. Maneno haya huwa na maana tofauti.Homografu ni za aina mbili:

#### 3.4.1 Homofoni

Homofoni ni homografu zinazotamkwa kwa namna sawa lakini zina maana tofauti. Pia maendelezo ya maneno haya huwa tofauti. Hatukuweza kupata mifano katika Kiswahili na Sheng labda ni kutokana na sababu kuwa kwa vile muundo wa Sheng hufanana na ule wa Kiswahili na lugha hizi sawa na lugha zingine za kibantu huchukua muundo wa KVKV katika maneno yao. Ni kutokana na hali hii ambapo muundo huu unapobadilishwa yaani maendelezo yakibadilishwa, matamshi ya neno hilo hubadilika pia. Hivyo maneno yatakayotokana na hali hii hayatakuwa homofoni.

#### 3.4.2 Heterofoni

Heterofoni ni homografu zilizo na muundo sawa lakini matamshi yao ni tofauti. Pia maana zao ni tofauti. Hatukuweza kupata mifano katika Sheng labda ni kutokana na sababu kuwa lugha hii haijaimarishwa na huenda ikawa na maneno yenye sifa hii jinsi wakati unavyozidi kusonga. Katika lugha ya Kiswahili tulibaini mifano ifuatayo:

34 a) Barabara-njia

b) Bara’bara-Sawasawa

Katika mfano huu maneno haya (a) na (b) ni heterofoni kwa sababu yana muundo sawa lakini matamshi yao ni tofauti, pia maana zao ni tofauti. Katika utafiti huu hatukuweza kupata mifano ya homografu katika Sheng labda jinsi wakati unavyozidi kusonga wanajamii lugha wa Sheng wataweza kuunda maneno yaliyo na uhusiano huu.

### 3.5 Kapitonimu

Kapitonimu ni mahusiano ambapo neno hubadilisha maana yake kila linapobadilika na kuwa herufi kubwa. Herufi kubwa yaweza kutumika kutofautisha jozi ya maneno. Maneno haya huwa na maumbo sawa lakini maana tofauti yanapoandikwa kwa herufi kubwa. Hatukupata mifano katika Sheng labda lugha hii itapata maneno yaliyo na uhusiano huu kadri inavyozidi kukua.

Mifano ya maneno katika lugha ya Kiswahili ni kama ifuatayo:

35 a) Mungu-Maulana

b) mungu-mojawapo ya miungu

c) Baba-Mtakatifu wa Roma

d) baba -Mzazi wa kiume

e) Bikira-Mama wa yesu

f) bikira-msichana ambaye hajashiriki mapenzi tangu utotoni

Kutokana na mifano hii tunabaini kuwa maneno Mungu na mungu ni kapitonimu kwa kuwa matumizi ya herufi kubwa katika mojawapo yameleta tofauti katika maana ya maneno haya. Pia hali hii inadhihirika katika maneno Baba na baba.

**3.6 Polisemia**

Upolisemia ni uhusiano wa maneno ambapo maneno hayo huwa na maana zaidi ya moja, Wamitila (2003). Maneno haya huwa na historia moja. Obuchi na Mukhwana (2010) nao wanaongezea kuwa umbo la neno moja huwa na maana mbalimbali. Tuliweza kushuhudia uhusiano huu katika utafiti huu wetu. Katika utafiti huu tulibaini mifano ya upolisemia katika lugha ya Kiswahili. Mifano hii ni kama ifuatayo:

36 a) Mdomo –wa mnyama

b) Mdomo –wa chupa

c) Mdomo –wa mtungi

d) Kata –Kitendo cha kukata

e) Kata –Kitambaa kilichoviringwa

f) Kata –Kamba iliyoviringwa

Kutokana na mifano hii maneno mdomo na kata yana maana zaidi ya moja, hivyo husemwa kuwa na mahusiano ya upolisemia.

Sheng pia ina mahusiano ya upolisemia na mifano ni kama ifuatayo:

37 a) Finga –Kidole cha mtu

b) Finga – ishara ya kujamiana

c) Finga – ishara ya matusi

d) Mshikaji –mpenzi wa kike

e) Mshikaji –mpenzi wa kiume

Kutokana na mifano hii maneno *finga* na *mshikaji* yana maana zaidi ya moja, hivyo yana mahusiano ya upolisemia.

**3.7 Antonimia**

Antonimia ni hali ambapo maneno huwa na maana kinyume cha maneno mengine, Wamitila (2003). Habwe na Nyonje (2010) nao wanasema kuwa antonimia ni uhusiano wa kimuundo ambapo maana ya maneno huwa vinyume. Uhusiano huu husaidia kupata maana ya neno kwa kutumia kinyume cha neno jingine. Tuliweza kubaini mifano ya mahusiano ya antonimia katika lugha ya Kiswahili. Mifano ni kama ifuatayo:

| | **Neno** | **Antonimu** |
|---|---|---|
| 38 | a) Moto – | Baridi |
| | b) Kubwa – | Dogo |
| | c) Ndani – | Nje |
| | d) Juu - | Chini |

Kutokana na mifano hii maneno katika mfano 38(a) ni vinyume, vivyo hivyo katika maneno 38(b), c na d. Kutokana na hali hii maneno haya husemwa kuwa yana mahusiano ya uantonimia.

Sheng nayo ina mahusiano ya uantonimia. Mifano ni kama ifuatayo:

| | **Neno** | **Antonimu** |
|---|---|---|
| 39 | a) Mathee(mama) | Fathee(baba) |
| | b) Chali(mvulana) | Manzi(msichana) |
| | c) Masa(mama) | Buda(baba) |
| | d) Kamu(njoo) | Zidi(enda) |

Kutokana na mifano hii maneno katika mfano (a) ni vinyume vivyo hivyo maneno katika (b). Hali hii hufanya maneno haya kusemwa kuwa na mahusiano ya uantonimia kwa kuwa yana sifa ya unyume.

### 3.8 Hitimisho

Katika sura hii tumeangazia mahusiano ya fahiwa katika maneno ya Sheng. Mahusiano ya fahiwa ni kigezo muhimu cha kisemantiki katika lugha yoyote. Tumebaini kuwa jinsi fahiwa hizi huhusiana na zingine katika lugha za Kiswahili, ndivyo hujitokeza katika Sheng. Mahusiano ya fahiwa tuliyoyabaini katika Sheng ni kama vile: haiponimia, sinonimia, homonimia, Polisemia na antonimia. Mahusiano haya husaidia kuelewa maana ya maneno katika lugha husika. Vifahiwa katika maneno ya lugha husababisha utata unaosababisha makosa ya kimaana hasa vinapotumika katika lugha nyingine. Tumeona kuwa baadhi ya maneno ya Sheng hupewa fahiwa tofauti na maana za maneno hayo katika lugha asilia, jambo hili huleta utata wa kimaana maneno hayo yanapotumiwa katika lugha zao asili hasa katika lugha ya Kiswahili hivyo kusababisha makosa ya kisemantiki. Uchambuzi wa data umetubainishia kwamba maneno ya Sheng humiliki na kuchangia kuwepo kwa mahusiano na hali mbalimbali zinazoathiri mikondo ya maana ya maneno. Hivyo ni dhahiri kuwa Sheng husababisha makosa katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili za Gusii Highlights na Daraja Mbili zilizoko mjini Kisii.

Makosa haya tutayajadili katika sura itakayofuata. Katika sura hii tutayaainisha makosa katika insha zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Makosa haya ni yale yanayotokana na Sheng.

# SURA YA NNE

# MAKOSA KATIKA KAZI ZA WANAFUNZI

## 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumetathmini mahusiano ya kisemantiki katika Sheng. Tumebaini kuwa uhusiano ambao neno linao na maneno mengine husaidia kupata maana ya neno hilo/maneno hayo. Katika sura hii ya nne tunadhamiria kuchanganua makosa katika insha zilizoandikwa na wanafunzi wa shule mbili za upili mjini Kisii pamoja na kueleza visababishi vyake. Pia tutaangazia mikakati ya kuzuia kutokea kwa makosa haya katika kazi za baadaye. Makosa haya ni yale yanayotokana na athari za Sheng. Lengo letu hapa ni kubaini iwapo Sheng husababisha makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Makosa katika matumizi ya Kiswahili sanifu ni matumizi ya Kiswahili yanayokiuka makubaliano ya kisarufi ya lugha ya Kiswahili. Swan na Smith (1987) wanasema kuwa makosa husababishwa na mwingiliano kati ya lugha mbili. Mwingiliano huo ndio husababisha utata katika matumizi ya lugha hivyo kusababisha makosa. Larsen (1992) naye anasema kuwa makosa huweza kuwekwa katika vitengo kadha. Vitengo hivi ni kama vifuatavyo: ujumlishaji wa kiholela, kutozingatia kanuni za lugha husika na ubunaji wa fikra zisizo za kweli. Mwandishi huyu anaongezea kuwa nadharia ya Uchanganuzi Makosa huchunguza idadi ya makosa ya wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili.

Tungo kadha tulizozichanganua zilidhihirisha kuwepo kwa makosa ya aina mbalimbali lakini utafiti huu ulijikita katika makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii yanayotokana na Sheng.

## 4.1 Makosa ya kimofolojia

Makosa ya kimofolojia hutokea wakati kanuni za uundaji wa maneno katika lugha husika hukiukwa. Makosa haya huweza kujitokeza katika kiwango cha mofu au hata neno zima. Makosa haya husababishwa na mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno ya Sheng.

Maneno ya Sheng yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hizi hujumuishwa katika lugha ya Kiswahili hivyo kuathiri miundo ya maneno. Hali hii husababisha makosa ya Kimofolojia. Katika utafiti huu tuliweza kupata makosa ya kimofolojia yanayotokana na mbinu za uundaji wa maneno ya Sheng kama zifuatazo.

### 4.1.1 Ukopaji

Makosa mengine ya kimofolojia yametokana na matumizi ya maneno yasiyo ya Kiswahili katika lugha ya Kiswahili. Maneno haya huwa yamekopwa kutoka lugha zingine na kutoholewa kabla ya kupitia mabadiliko mengine. Mifano ya maneno haya ni kama ifuatayo:

40 a) *Princi alitugotea vipoa.(*Mwalimu mkuu alitusalimia vizuri.)

*b) Afta kumaliza kiamsha kinywa nilijikata.(*Baada ya kumaliza kiamsha kiywa niliondoka.)

*c)Tulipata fom ata kuskia kuna jam tulizidisha tu. (*Tulipata mpango hata kusikia kuna msongamano wa magari tuliharakisha tu.*)*

*d) Alafu makarao wakakam.(*Halafu polisi wakaja.)

Kutokana na mifano hii maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiingereza ni kama vile: *princi*, *afta* na *fom*. Mengine yamekopwa kutoka lugha ya Kikikuyu kama vile neno *mathaa*. Maneno haya baaada ya kukopwa yametoholewa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa Sheng. Kwa mfano neno *princi* baada ya kukopwa kutoka kwa neno *principal* la Kiingereza limefanyiwa ukatizaji tamati. Licha ya ukopaji huu maana zinazopewa maneno haya katika Sheng hufanana na maana za maneno haya katika lugha changizi.

### 4.1.2 Ubunaji

Ubunaji wa maneno katika lugha moja ili kuelezea dhana au hali fulani husababisha makosa ya kimofolojia maneno hayo yanapotumika katika lugha nyingine. Sheng hutumia mbinu ya ubunaji kujiundia leksemu zake na ndivyo ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Maneno yaliyobuniwa kwa matumizi katika Sheng yanapotumiwa katika kazi za Kiswahili hudhihirika kama makosa ya kimofolojia. Katika utafiti huu tulibaini

maneno yaliyobuniwa kwa matumizi katika Sheng yaliyotumiwa katika kazi za Kiswahili. Mifano ni kama ifuatayo:

41 a) *Buda alikuwa atupe ndai yake.(*Baba alikuwa atupe gari yake.)

*b) Niliwaambia arif zangu tujikate.(*Niliwaambia rafiki zangu tuondoke.)

*c) Mazee kidogo ivi tulipata…(*Jamani kidogo hivi tulipata…)

*d) Orogram yangu ikaanguka na kuspoil.(*Simu yangu ikaanguka na kuharibika.)

Kutokana na mifano maneno yaliyobuniwa kwa matumizi katika Sheng yaliyotumiwa katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi hawa ni kama vile : *makarao, mudenge, orogram, mazee, arif* na *ndai*. Matumizi ya maneno haya hudhihirika kama makosa ya kimofolojia.

### 4.1.3 Uambishaji

Baadhi ya makosa ya kimofolojia yametokana na uambishaji usiofaa katika maneno ya Kiswahili. Mofu zinazoongezwa katika maneno haya hutumiwa kuleta maana fulani. Uhamishaji huu hutokana na uhamishaji wa kanuni za Sheng katika lugha ya Kiswahili. Makosa ya kimofolojia hutokea pale ambapo maneno ya Sheng yaliyokopwa na kuambishwa,hutumiwa katika lugha ya Kiswahili. Mifano ya maneno haya ni kama vile:

42 a) *Maarif zangu walinipa tuzawadi.(*Marafiki zangu walinipa vijizawadi.)

*b) Mavijana wakatokolezea.(*Vijana wakatokezea.)

*c) Mademu wa chuo jirani walipowasili.(*Wasichana wa shule jirani walipowasili.)

Kutokana na mifano hii maneno yaliyoongezewa viambishi ni kama vile *mavijana*, *tuzawadi*, *tokelezea* na *mademu*. Mofimu{ma}huwakilishahali ya wingi, mofimu {le}huwakilisha hali ya kutendea na mofimu {tu}huwakilisha hali ya udogo au udunishaji.

### 4.1.4 Upolisemia

Baadhi ya makosa ya kimofolojia katika maneno yametokana na mbinu ya upolisemia. Katika sura ya pili tulieleza maana ya upolisemia kuwa upolisemia ni mbinu ya uundaji maneno inayohusu upanuzi wa maana ya maneno ambayo tayari yako katika lugha.

Mifano ifuatayo inaonyesha maneno ya Kiswahili yaliyopanuliwa kimaana kwa matumizi katika Sheng.

43 a) *Ju walikuwa supu kuruka.(*Kwa sababu walivutia ajabu.)

*b) Alitugotea vipoa.(*Alitusalimiavizuri.*)*

Maneno kama *supu*, *gota na poa* yameundwa kutokana na mbinu hii ya upolisemia. Maneno haya huwa yamekopwa kutoka lugha ya Kiswahili na kupanuliwa kimaana ili kupata maana mpya. Kwa mfano maana asili ya neno *gota* katika lugha ya Kiswahili linamaanisha kitendo cha kugonga kwa kutumia sehemu ya nyuma ya mkono. Neno hili katika Sheng limepanuliwa na kupewa maana mpya yaani kusalimia kwa kutumia sehemu ya nyuma ya mkono. Pia neno *poa* katika lugha asilia ya Kiswahili linamaanisha hali ya kitu kilichokuwa moto kuwa baridi. Neno hili limepanuliwa kimaana na kupewa maana mpya katika Sheng ambayo ni vizuri. Neno supu katika lugha ya Kiswahili lina maana ya mchuzi au rojorojo neno hili katika Sheng limepanuliwa kimaana na kutumiwa kwa maana ya kuvutia. Maneno haya ya Sheng yanapotumiwa katika lugha ya Kiswahili kwa maana ile ya Sheng huchukuliwa kuwa makosa ya kimofolojia.

Maneno na miundo ya Sheng hutumiwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Sababu za kutokea kwa hali hii ni kama vile: mazoea ya kutumia Sheng badala ya Kiswahili sanifu, wengi huchanganyikiwa wasijue ni maneno yapi yaliyo ya Sheng na yapi yaliyo ya Kiswahili sanifu na wengine husahau miktadha ya matumizi ya Kiswahili sanifu na Sheng.

Makosa haya ya kimofolojia tuliyachanganua kitakwimu kwa kuyatafutia asilimia zao ili kubaini ni wanafunzi wa vidato vipi wanaoathirika zaidi ya wengine katika shule hizi za upili mjini Kisii. Ili kuweza kuchanganua makosa haya, tulihesabu idadi ya makosa haya katika kila kidato na hatimaye kujumuisha idadi ya vidato vyote. Kisha tulitafuta asilimia ya makosa katika kila kidato kama ifuatavyo:

Idadi ya jumla ya makosa ya kimofolojia = 680

Idadi ya makosa katika kidato cha 4 =280 Asilimia 41.7%

Idadi ya makosa katika kidato cha 3 =206 Asilimia 30.3%

Idadi ya makosa katika kidato cha 2 =110 Asilimia 16.5%

Idadi ya makosa katika kidato cha 1 =84 Asilimia 12.3%

Katika utafiti huu tulibaini kuwa wanafunzi walio katika vidato vya juu huwa na asilimia kubwa ya makosa wakilinganishwa na wale walio katika vidato vya chini. Wanafunzi wa kidato cha nne walikuwa na asilimia 41.7% ya makosa wakifuatiwa na wale wa kidato cha tatu waliokuwa na asilimia 30.3% kisha wale wa kidato cha pili waliokuwa na asilimia 16.5% na mwisho wanafunzi wa kidato cha kwanza waliokuwa na asilimia 12.3% ya makosa ya kimofolojia.

Hali hii inaonyesha kwamba, jinsi mwanafunzi anavyoendelea kuwa shuleni, ndivyo anavyozidi kuathirika kutokana na Sheng. Sababu za kutokea kwa hali hii ni kwamba baadhi ya walimu wanaofunza somo la Kiswahili ambao ni vijana kiumri hutumia Sheng wanapowasiliana na wanafunzi hivyo kufanya wanafunzi walioingiliana na walimu hawa kwa muda mrefu kuathirika zaidi kuliko wale walioingiliana na walimu hawa kwa muda mfupi kwa sababu wanafunzi hawa huwaiga walimu wao. Vilevile kutokana na ukomavu wa wanafunzi hawa katika Sheng, huwafanya kutumia lugha fiche isiyoeleweka na wengi katika mawasilano yao. Hali hii hufanya wanafunzi wa vidato vya juu kuathirika zaidi kutokana na Sheng kuliko wale walio katika vidato vya chini.

### 4.2 Makosa ya Kisemantiki

Makosa ya kisemantiki ni makosa yanayoathiri maana za maneno, virai na sentensi za lugha fulani. Makosa haya hutokea wakati fahiwa tofauti hupewa maneno ya lugha husika kinyume na kanuni za kisarufi za lugha hiyo. Makosa haya yanapoathiri maana za maneno katika sentensi, basi maana ya sentensi zima huathirika. Katika utafiti huu tulibaini kuwa baadhi ya fahiwa hizi hutokana na mahusiano ya upolisemia. Katika sura ya tatu tulieleza mahusiano ya upolisemia kuwa ni hali ambapo maneno huwa na maana zaidi ya moja. Neno linapokuwa na maana zaidi ya moja husababisha utata wa kimaana hivyo kusababisha makosa ya kisemantiki maana hizi zinapohusishwa katika miktadha mbalimbali. Katika utafiti huu tulibaini kuwa wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii

hufanya makosa ya kisemantiki yanayotokana na Sheng kwa sababu ya mahusiano ya upolisemia. Maneno ya Sheng yenye sifa hii ya upolisemia huwa yamekopwa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno haya baada ya kukopwa huwa hayapitii mabadiliko yoyote bali hutumiwa jinsi yalivyo katika lugha pokezi(Sheng). Makosa haya hutokana na fahiwa mbalimbali zinazopewa maneno yenye asili ya Kiswahili yanayotumiwa katika Sheng. Katika utafiti huu tulibaini mifano ya makosa ya kisemantiki ifuatayo:

44 a) *Afta kumaliza niliwaambia ma arif zangu tujikate.(*Baada ya kumaliza niliwaambia marafiki zangu tuondoke.)

*b) …ata kuskia kuna jam tulizidisha tu. (…*hata kusiki akuna msongamano wa magari tuliharakisha tu.)

*c)Tulishtuka sana juu tulijua tumepatwa na muhadhara.*(Tulishtuka ana kwa sababu tulijua tumepatwa na matatizo.)

*d) …maboiz wetu waliwadandia juu walikuwa supuu kuruka.(…*wavulana wetu waliwakwamilia kwa sababu walivutia ajabu.)

*e)…alinipa noti ya ngiri na kuishia.(…*alinipa noti ya elfu moja na kwenda.)

*f) Aliamua kuwaruka wote.(*Aliamua kuwakataa wote.)

Kutokana na mifano hii tumebaini kuwa baadhi maneno ya Kiswahili yanapokopwa na kutumiwa katika Sheng hupewa fahiwa tofauti. Hali hii imejitokeza katika mfano huu. Katika mfano (a) neno *kujikata* katika Kiswahili lina maana ya kujiumiza kwa kifaa chenye makali lakini katika Sheng neno hili lina maana ya kuondoka. Neno hili linapotumika katika lugha ya Kiswahili kwa maana ile ya Sheng hupotosha maana iliyokusudiwa na hivyo kudhihirika kama kosa la kisemantiki.

Neno *zidisha* katika mfano (b) katika lugha ya Kiswahili, lina maana ya kupitisha kiasi lakini katika Sheng neno hili lina maana ya kuharakisha. Vivyo hivyo neno *juu* katika (c) lugha ya Kiswahili lina maana ya sehemu ya juu lakini katika Sheng neno hili lina maana ya sababu. Pia hali hii hujitokeza katika neno *mhadhara* katika lugha ya Kiswahili ambalo lina maana ya kikao cha usomi ilhali katika Sheng lina maana ya matatizo. Maneno mengine yaliyotumiwa yenye mahusiano ya upolisemia ni kama vile*ruka*, *ishia*,

*kuruka na dandia*. Maneno haya yaliyo na maana zaidi ya moja yanapotumiwa katika lugha ya Kiswahili kwa ile maana ya Sheng huzua utata wa kimaana hivyo, maana inayojitokeza katika sentensi husika hupotoka.

Neno *ruka* katika lugha ya Kiswahili humaanisha hali ya kuelekea sehemu iliyo juu lakini katika Sheng neno hili limepewa maana zaidi na linatumika kwa maana ya kukataa. Vilevile neno ishia katika Kiswahili lina maana ya hali ya kitu kutotosha lakini katika Sheng neno hili limepewa maana zaidi nayo ni kwenda.

Makosa haya ya kisemantiki tuliweza kuyachanganua kitakwimu ili kupata asilimia za makosa hayo na pia kubaini wanafunzi wanaoathirika zaidi kutokana na Sheng. Ili kuchanganua makosa haya, tulihesabu makosa ya kisemantiki katika kila kidato kisha makosa haya kwa ujumla. Kwa kufanya hivi tuliweza kupata asilimia ya makosa katika kila kidato kama ifuatavyo:

Idadi ya jumla ya makosa ya kisemantiki=288

| | | |
|---|---|---|
| Idadi ya makosa katika kidato cha 4 | =120 | Asilimia 41.6% |
| Idadi ya makosa katika kidato cha 3 | =88 | Asilimia 30.6% |
| Idadi ya makosa katika kidato cha 2 | =56 | Asilimia 19.4% |
| Idadi ya makosa katika kidato cha 1 | =24 | Asilimia 8.3% |

Tulibaini kuwa makosa mengi ya kisemantiki hufanywa na wanafunzi wote lakini kwa asilimia tofauti. Wanafunzi wa kidato cha nne walikuwa na asilimia 41.6% ya makosa ya kisemantiki, wakifuatiwa na wale wa kidato cha tatu waliokuwa na asilimia 30.6%,kisha wanafunzi wa kidato cha pili waliokuwa na asilimia 19.4% na mwisho wale wa kidato cha kwanza waliokuwa na asilimia 8.3%.

Hali hii ya kutokea kwamakosa ya kisemantiki inatokana na sababu kwamba Sheng ni lugha inayobadilikabadilika kila uchao hivyo, maneno yake hupewa fahiwa tofauti tofauti kila uchao. Jinsi wanafunzi wanavyozidi kukomaa kiumri ndivyo wanavyozidi

kuzifahamu fahiwa hizi hivyo kufanya makosa mengi ya kisemantiki yanayotokana na Sheng.

Pia makosa mengi ya kisemantiki yanayotokana na Sheng hufanywa na wanafunzi wa vidato vya juu kwa sababu ya ukomavu wao katika lugha hii. Ukomavu huu hutokana na sababu kuwa wengi wa wanafunzi hawa hushindana ili kubaini ujuzi wa kila mmoja wao katika lugha hii ya Sheng. Hali hii ya ushindani hufanya lugha ya Sheng na Kiswahili kushindania nafasi moja katika akili za wanafunzi hawa, hivyo kuwatatanisha zaidi kila wanapohitajika kutumia Kiswahili sanifu. Hali hii ni tofauti katika wanafunzi wa vidato vya chini ambao kwa wakati mwingi hukipa Kiswahili nafasi ya kwanza kwa vile huwa hawajaimudu Sheng.

Kutokana na utafiti huu, tumeweza kubaini kuwa, makosa ya kimofolojia ni mengi kuliko makosa ya kisemantiki yanayotokana na Sheng katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Hali hii inatokana na sababu kwamba baadhi ya maneno ya Sheng yanayosababisha makosa ya kimofolojia yanapotumika katika Kiswahili sanifu(lugha changizi), huwa na maana sawa katika Sheng (lugha pokezi). Hivyo,kwa wanafunzi hawa wa shule za upili mjini Kisii  makosa ya kisemantiki huwa machache yakilinganishwa na yale ya kimofolojia.

### 4.3 Mikakati ya Kuzuia Makosa Yanayotokana na Sheng

Katika utafiti huu walimu wa somo la Kiswahili walionekana kukubaliana kuwa wanafunzi huchanganya Sheng na Kiswahili kila wanapohitajika kutumia Kiswahili sanifu. Walipendekeza mikakati mbalimbali inayofaa kuzingatiwa ili kuzuia makosa katika lugha ya Kiswahili yanayotokana na Sheng.

#### *4.3.1 Kupigia kistari neno/maneno yenye makosa*

Mwalimu anapoisoma na kuihakiki kazi ya mwanafunzi, neno lililo na kosa hupigiwa kistari kisha jibu sahihi huandikwa juu yake. Mbinu hii itamfaa mwanafunzi anapoipitia tena kazi ile kwani ataweza kugundua kosa lile na jibu lililostahili hivyo hatarudia  tena baaadaye kosa lile.

### *4.3.2 Kusisitiza nafasi na umuhimu wa Kiswahili sanifu*

Mbinu hii inafaa kutumiwa na walimu na wanafunzi shuleni. Walimu wanafaa kuweka vikwazo dhidi ya matumizi ya Sheng shuleni pia kuwaeleza wanafunzi umuhimu wa mazoea ya kutumia Kiswahili sanifu. Vilevile hali ya kuwatuza wanafunzi wanaotumia Kiswahili sanifu itawatia motisha wanafunzi wengine kufanya hivyo ili nao waweze kufaidi tunu.

### *4.3.3 Kuweka mabango shuleni yanayokejeli matumizi ya Sheng*

Mbinu hii inahusisha kuweka mabango shuleni kwenye sehemu zilizo wazi yanayoonyesha ubovu wa Sheng. Makosa ambayo tayari yamepatikana katika kazi za wanafunzi yafaa kuandikwa kwenye mabango haya ili kila mwanafunzi aweze kuyaona. Mbinu hii itasaidia wanafunzi kuepuka makosa kama hayo katika kazi zao zinazofuata.

### *4.3.4 Walimu kushiriki mazungumzo na wanafunzi*

Walimu wanafaa kuchukua jukumu la kushirikisha wanafunzi wao katika mazungumzo kuhusu athari za Sheng katika somo la Kiswahili. Hali hii itawafanya walimu kutambua mielekeo ya wanafunzi kuhusu Sheng. Pia walimu hawa wataweza kutambua makosa ya wanafunzi hivyo kuyarekebisha ifaavyo.

### *4.3.5 Kuwaita wanafunzi na kuwarekebisha papo hapo*

Baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi na kutambua makosa, walimu wanafaa kuwaita wanafunzi wenye matatizo ya Kiswahili yanayotokana na Sheng na kuwarekebisha papo hapo. Hali hii itawafanya wanafunzi kutoyarudia makosa hayo tena. Kwa njia moja au nyingine, wanafunzi hawa watahisi wamekejeliwa kwa kukosolewa hadharani na ili kuepuka kejeli kama hii katika siku za usoni, watajirekebisha.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumebaini kuwa wanafunzi hufanya makosa mbalimbali katika kazi zao za Kiswahili. Makosa haya hutokea katika viwango vya mofolojia na semantiki. Baadhi ya makosa haya kwa lugha ya Kiswahili hutokana na athari za Sheng. Wanafunzi katika vidato vyote vya shule za upili mjini Kisii huathirika na Sheng na hivyo makosa haya hudhihirika katika kazi zao za Kiswahili zilizoandikwa. Utafiti huu ulionyesha kuwa

wanafunzi walio katika vidato vya juu huathirika zaidi kuliko wale walio katika vidato vya chini kutokana na sababu kama vile mazoea ya kutumia Sheng kwa muda mrefu na athari kutoka kwa walimu wanaofunza lugha ya Kiswahili wanaotumia Sheng wanapofunza. Tulibaini kuwa makosa haya husababishwa na mambo kadha kama vile: mbinu mbalimbali za uundaji wa leksemu za Sheng kama vile ubunaji, ukatizaji na ukopaji. Makosa mengine hutokana na mahusiano ya upolisemia katika maneno yenye asili ya Kiswahili yanapotumiwa kwa maana ya Sheng. Isitoshe tulibaini mikakati mbalimbali inayofaa kutumiwa na walimu wa Kiswahili kuzuia makosa yanayotokana na athari za Sheng. Mikakati hii ni kama ifuatayo: kupigia kistari neno lenye/maneno yenye makosa na kuandika neno sahihi juu yake, kusisitiza nafasi na umuhimu wa kutumia Kiswahili sanifu, kuweka mabango yanayokejeli matumizi ya Sheng mahali yanapoweza kuonekana shulenina kushiriki mazungumzo na wanafunzi kuhusu mapungufu ya Sheng kama msimbo na athari zake hasi kwa Kiswahili.

Katika sura ifuatayo tutaweza kutoa muhtasari wa kazi yote, mahitimisho na mapendekezo ya tafiti zinazofaa kufanywa katika siku za baadaye.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Muhtasari

Katika sura ya nne tulishughulikia uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wa shule mbili za upili mjini Kisii. Tulikita uchanganuzi wetu katika makosa ya kimofolojia na kisemantiki yanayotokana na Sheng katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi hawa. Katika sura hii tumetoa muhtasari wa kazi yote, mahitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti huu. Yote haya yalifungamana na malengo ya utafiti huu ambayo tulitaka kuyafikia mwishoni mwa utafiti huu.

Athari za Sheng katika jamii lugha ya Kikisii ni nyingi na zinaendelea kukua na kukita mizizi kila uchao. Tuliamua kukita katika athari za Sheng katika elimu ya shule za upili kwa sababu kiwango cha shule za upili ni kiwango muhimu katika mfumo wa 8-4-4 nchini Kenya. Pia kiwango hiki huhusisha vijana ambao kwa kiasi kikubwa huhusishwa na matumizi ya Sheng katika mawasiliano yao.

Katika sura ya pili tumeangazia mbinu mbalimbali za kimofolojia ambazo Sheng huzitumia katika uundaji wa leksemu zake. Mbinu hizi huwa bia hivyo basi hutumiwa na lugha nyingi katika kujiundia leksemu zao ili ziweze kujitosheleza kimsamiati. Mbinu tulizozibaini ni kama vile: ukopaji, uambishaji, unyambulishaji, onomatopia, ubunaji, ukatizaji, uambatanishaji na upolisemia. Uundaji huu wa leksemu za Sheng ndio huwa chanzo cha athari zinazosababisha makosa ya kimofolojia katika lugha ya Kiswahili.

Katika sura ya tatu tumetalii jinsi ambavyo Sheng hutumia leksemu mbalimbali iliyojiundia kwa kujiundia vifahiwa kadha. Mahusiano ya vifahiwa hivi hutumiwa na wanajamii lugha wa Sheng kuzipa leksemu hizi maana mbalimbali. Mahusiano haya ni pamoja na: haiponimia, sinonimia, homonimia, polisemia na antonimia. Vifahiwa hivi tumevijadili kwa kina ili kuziweka bayana sifa zake pamoja na utendakazi wake. Vifahiwa hivi vya Sheng ndivyo huleta utata wa kimaana hasa vinapotumiwa katika lugha ya Kiswahili. Utata huu hupotosha maana ya maneno na sentensi zima katika lugha

ya Kiswahili. Utata huu husababisha makosa ya kisemantiki yanayopelekea matokeo duni katika somo la Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.

Katika sura ya nne tumechanganua makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika insha za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule mbili za upili mjini Kisii. Sababu ni kwamba utafiti huu ulitaka kutathmini athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii. Hivyo tumepata kubaini kwamba Sheng ina athari katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa vidato vyote ila wanafunzi walio katika vidato vya juu huathirika zaidi kuliko wale walio katika vidato vya chini. Hali hii hutokana na sababu kwamba wanafunzi walio katika vidato vya juu wana ujuzi mwingi wa lugha hii kutokana na matumizi ya lugha hii kwa muda mrefu kuliko wale walio katika vidato vya chini. Vilevile wanafunzi walioingiliana na walimu wanaofunza somo la Kiswahili ambao hutumia Sheng katika mawasiliano yao kwa muda mrefu huathirika zaidi kuliko wale walioingiliana na walimu hawa kwa muda mfupi.

## 5.1 Mahitimisho

Utafiti huu ulikuwa unachanganua makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili za Gusii Highlights na Daraja Mbili. Makosa haya ni yale yanayotokana na Sheng. Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa makosa haya. Makosa haya hujitokeza katika kazi za wanafunzi wa vidato vyote japo kwa asilimia tofauti tofauti. Utafiti huu umebainisha kuwa kadri mwanafunzi anavyoendelea na masomo katika vidato vya juu ndivyo makosa haya huendelea kuongezeka. Hali hii hufanya wanafunzi katika vidato vya juu kuwa na makosa mengi kuliko wale walio katika vidato vya chini. Sababu za kutokea kwa hali hii ni pamoja na uhamishaji wa ufundishaji, hali ambapo wanafunzi huwaiga walimu wanaotumia Sheng katika mawasiliano yao na ujumlishaji wa kanuni za Sheng katika lugha ya Kiswahili.

Malengo ya utafiti huu yameafikiwa na matokeo ya utafiti. Lengo la kwanza lililenga kubaini iwapo Sheng husababisha makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Utafiti huu ulibainisha kuwa Sheng husababisha makosa ya kimofolojia na kisemantiki katika kazi za

Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii. Wanafunzi hutumia miundo ya Sheng katika maneno ya Kiswahili. Pia wanafunzi hawa hutumia baadhi ya maneno ya Sheng katika lugha ya Kiswahili. Isitoshe baadhi ya wanafunzi hutumia vifahiwa vya Sheng kwa maana ya Kiswahili. Haya yote ni makosa yanayosababisha matokeo duni katika lugha ya Kiswahili.

Lengo la pili lilikuwa kubaini iwapo wanafunzi katika vidato vyote huathirika kutokana na Sheng kwa namna sawa. Utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi walio katika vidato vya juu huathirika zaidi kuliko wale walio katika vidato vya chini. Baadhi ya sababu za kutokea kwa hali hii ni kwamba, baadhi ya walimu hutumia Sheng katika mawasiliano yao wanapowasiliana na wanafunzi. Hali hii hufanya wanafunzi ambao wameingiliana na walimu hawa kwa muda mrefu, hasa wale wa vidato vya juu,kuathirika zaidi kuliko walioingiliana na walimu hawa kwa muda mfupi ambao ni wale wa vidato vya chini.

Lengo la tatu lilikuwa kubaini iwapo nadharia ya Uchanganuzi Makosa inafaa katika kutathmini makosa ya wanafunzi katika somo la Kiswahili. Katika utafiti huu tulibaini kuwa nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilitufaa pakubwakwa kuwa tuliweza kutumia mbinu zilizopendekezwa katika nadharia hii kuainisha na kurekebisha makosa yanayotokana na Sheng katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili mjini Kisii.

Nadharia za Uchanganuzi Makosa na Lugha Kadirifu zimetufaa katika utafiti huu. Tumefuata hatua zilizopendekezwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa katika kuchanganua data. Baada ya kutambua makosa katika kazi za wanafunzi tuliyaainisha makosa yale katika kategoria mbalimbali na kueleza visababishi vya makosa yale.nadharia ya Lugha Kadirifu ilitufaa katika kuelewa baadhi ya visababishi vya makosa katika lugha ya pili ya mwanafunzi. Visababishi hivi ni kama vile: uhamishaji wakanuni za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili na ujumlishaji mno.

Kutokana na sababu hizi wanafunzi hufanya vibaya katika somo la Kiswahili hivyo kusababisha matokeo duni.

## 5.2 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kutathmini athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii. Hivyo basi, tumeweza kubaini kuwa Sheng huathiri utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili mjini Kisii. Hali hii husababisha matokeo duni katika somo la Kiswahili katika shule za upili mjini Kisii. Athari hizi huenda zikawa tofauti katika miji mingine nchini Kenya. Hivyo tafiti zingine zinafaa kufanywa kuhusu athari za Sheng katika miji mingine midogo midogo nchini Kenya ili kubaini athari na maenezi ya lugha hii ikizingatiwa kwamba leksemu za Sheng hutofautiana kulingana na maeneo ambapo lugha hii huzungumzwa. Pia utafiti huu ulijikita katika shule za upili, hivyo tafiti zaidi zinafaa kufanywa katika viwango vingine vya elimu kama vile vyuo vya ualimu na vyuo vikuu nchini Kenya ili kubaini athari za Sheng katika viwango hivi. Labda tafiti hizi zitasaidia kupata suluhu kuhusu hatari hii ya walimu kutumia Sheng katika miktadha rasmi kama vile shuleni hata darasani.

# MAREJELEO


Abdulaziz, M. H na Osinde, K. (1997) ‘*Sheng and Engsh. Development of mixed codes among the urban youth in Kenya.’ International Journal of the Sociology of Language*.125:43-65.

Akoth, B. (2015) Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi*:* Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili na Kisuba. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.

Amanda, L. (2011) ‘Pohamba’s Namlish Offers Light Relief.’ The Namibian. August 12.

Buliba, A. Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006) *Isimu Jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Briton, L. J. (2000) *The Structure of Modern English*. *A Linguistic Intro Illustrated Edition*. John Benjamin Publishing Company.

Corder S. P. (1981) *Error Analysis*. London. Longman Publishers.

Corder, S. P. (1967) *Error Analysis and Interlanguage.* Oxford. Oxford University Press.

Crystal, D. (1980) *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. New York. Bluckid Publisher.

Echessa, P. G. (1990) A Study of the Word Structure and Processes involved in Word Formation in Sheng. A case study of Eastlands area in Nairobi. Unpublished Masters thesis. UON.

Edmonds, P. (2005) ‘*Word Sense Dis Ambiguation.’* The Elsevier Encyclopedia of language and linguistics. Oxford. Elsevier.2nd ed 607-623.

Fromkin, V. na Rodman,R. (1993) *An Introduction to Language.* Canada. Thomson Wadsworth.

Gass, S. na Selinker, L. (2008) *Second Language Acquisition*: *An Introductory Course*. New york. Routledge.

Githiora, J. (2002) 'Sheng; Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole?' Journal of African Cultural studies. University of London vol.15 pp159-183.

Githinji, P. (2006) Sheng and Variation. The Construction and Negotiation of Layered Identities. Unpublished Phd dissertation. Michigan State University.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya sarufi ya Kiswahili.* Nairobi. Phoenix Publishers.

Habwe, J. Asumpta, M. na Nyonje, J. (2010) *Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyuo.* Nairobi. Phoenix Publishers.

Hartman, R.. K, and Stork F. C. (1972) *Dictionary of Languages and Linguistics.* London: Applied science Publishers.

Iribemwangi na Mukhwana, A. (2011) *IsimuJamii*. Nairobi. Focus Publishers.

Kachipela, D. (2014) Athari za Sheng katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi mtaa wa Kangemi. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.

Katamba , F. (1993) *Morphology*. Cambridge. Cambridge University Press.

Kitsao, R.. (2015) Uchanganuzi wa Makosa ya Kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi na yanavyochangia matokeo mabaya ya mitihani, Kata ya Ganze, Kaunti ya Kilifi, Kenya. Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Pwani.

Kobia, J. (2006) 'Sheng is not a Language but Popular Slang.' Sunday Nation, Nairobi Feb. 2.

Lado, R.. (1957) *Linguistic Across Cultures*. Anne Arbo University. Michigan Press.

Larsen, M. H. (1992) *An Introduction to Language Two Acquisition Research.* Longman. London.

Lave, J. na Wenger, E. (1991) '*Situated Learning*: *Legitimate Peripheral Participation*.' Academic Search.

Lee, W. (1980) *Thoughts on Contrastive Linguistic in Context of Language Teaching.* Allatis. Washington.

Mahu, F. (2009) 'Leave Sheng to Matatu Touts and Musicians. The Standard, September 29

Mazrui, A. M. (1995) 'Slang and Code Switching: The case of Sheng in Kenya.' Africanistich Arbeitspapier 42:16-179.

Mbaabu, I. (2003) *Sheng-English Dictionary*. University of Dar es salaam. TUKI.

Mbaabu, I. na Nzunga, K. (2003) *English-Kiswahili Dictionary of Sheng*. *Deciphering East Africa Underworld Language*. Dar es salaam. TUKI.

Mkangi, K. (1984) 'Sheng and the Kenyan culture.' The Standard. August. 30.

Moga, J. na Fee, D. (1997) *Sheng Dictionary.* Nairobi. Ginsen Publishers.

Momanyi, C. (2009) 'Effects of Sheng in the Teaching of Kiswahili in Kenyan schools.' Journal of Pan African studies. 12:127-128.

Mpande, M. (1990) 'Sheng and the Kenyan Culture.'The Standard, Nairobi, August 30.

Mugenda, O. M. na Mugenda, A. G. (1999) *Research methonds: Quantitative and Qualitative Approaches.* African center for Technology studies. Nairobi.

Mukhebi, l. (1986) 'Is Language and Culture Inseparable?' Kenya Times, Nairobi, May 28.

Mweri, J. G. (2010) *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ndiku, L, Mwita, M. na Ocharo, G, (2014) Student and Educator Perceptions of use of Sheng. Unpublished B. A. University of East Africa.

Ngesa, M. (2012) 'And Sheng lives on Profile' . East African Standards 16-22Feb. 2012.

Nguemo, T. M. (2008) ‘The Prevalence of Slang use among students of Basic remedial studies and its effects on the Teaching of English as a second language.’ Ahmadu Bello University.

Njoroge, F. (2014) Hali, hadhi na Majukumu ya Sheng mjini Nakuru. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.

Obara, J. (2014) Uchanganuzi wa Makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.

Obuchi, M. S na Mukhwana, A. (2010) *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na vipengele.* Nairobi. Frame publishers.

Odhiambo, G. (2013) Athari za Sheng katika Dini ya Kikiristo mtaa wa Umoja. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.

Ogechi, N. O. (2002) Trilingual Code Switching in Kenya. Evidence from Ekegusii Kiswahili, English and Sheng. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Hamburg. University of Hamburg.

Ogechi, N. O. (2004) ‘On Lexicalization in Sheng.’ Nordic Journal of African Studies.Vol 2:325-342.

Ogechi, N. O. (2005) ’Does Sheng have a Kiswahili grammer?’ AP.A.L Annual Publication in African linguistics.3.3-25.

Okoto, W. L. (2015) Athari za Sheng kwa lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.

Osinde, K. (1986) Sheng; An investigation into the Social and Structural Aspects of an Evolving Language. Tasnifu ya B. A ambayo bado haijachapishwa. UON.

Richards et al. (1985) *Longman Dictionary of Applied Linguistics.* UK. Longman Group.

Sabiti, B. (2015) ’One of the Funniest and Strangest English Varieties in the World.’ Daily Monitors, February 20.

Selinker, L. (1969) *Language Transfer*. *General linguistics.* Newyork. Rawlence Eribaum Associates.

Selinker, L. (1972) *Interlanguage*. New york. Rawlence. Eribaum Associates.

Shitemi, N. L. (2001) 'Pidginization: Sheng the melting pot of Kenyan Languages and an Anti-Babel Development.' Dar es salaam. Institute of Kiswahili Research.

Spyropoulos, M. (1987) 'Sheng Some Preliminary Investigation into a Recently Emerged Nairobi Street Language.' Journal of the anthropological society. Oxford 18(2) 125-136.

Swan, M. & Smith, B. (1987) *Learners English: A teacher's Guide to Interference and other Problems.* Cambridge. Cambridge University Press.

Waithira, C. (2011) Astudy of the structure of the youth jargons in Nairobi. Unpublished Phil. thesis. Moi University.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi na Nadharia.* Nairobi. Focus Books.

Warambo, P. (2011) Uchanganuzi wa Maendeleo ya Kisematiki katika Sheng: Mtazamo wa Pragmatiki Leksika. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.

Webb na Kembo-Sure (1992) *African Voices*; *An Introduction to the Languages and Linguistics of Africa*. Cape Town and New York. Oxford University Press.

# KIAMBATISHO A.

## HOJAJI

Mimi ni Lydiah Nyambeki Mekonge, mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi.Nimekuja kufanya utafiti kuhusu Athari za Sheng katika ufundishaji wa Kiswahili.Kazi hii ni kwa ajili ya kitaaluma. Mchango na maoni utakayotoa yatakuwa ya manufaa makubwa kwangu na wale watakaoisoma kazi hii.Maoni yako yatakuwa siri kubwa.Karibu

**SEHEMU A**

(Tumia alama × kuonyesha jibu lako)

1. Matokeo ya mitihani katika somo la Kiswahili katika siku za hivi karibuni yanaridhisha.

   (a)Nakubali kabisa

   (b)Nakubali

   (c)Sikubali

   (d)Sikubali kabisa

2..Je, uwezo wako kama Mwalimu wa kuzungumza na kuelewa sheng ni wa kiwango gani?

a) Mzuri sana
b) Mzuri
c) Kiasi
d) Mbaya
e) Mbaya sana

3..Wanafunzi katika shule yako wanachanganya matumizi ya Sheng na kiswahili katika kazi zao za Kiswahili.

a)Nakubali kabisa

b)Nakubali

c)Sikubali

d)Sikubali kabisa

4..Kati ya wanafunzi wa vidato vyote vinne, ni wapi wanaoathirika zaidi na Sheng?

a) Kidato cha tatu na nne
b) Kidato cha kwanza na pili
c) Wote
d) Hakuna

5. Walimu shuleni mwako hutumia sheng katika mawasiliano yao

a) Nakubaliana kabisa
b) Nakubali ✓
c) Sikubali
d) Sikubali kabisa

**SEHEMU B**

1. (a)Ni lugha zipi zinazotumiwa katika mawasiliano shuleni mwako?

kingereza kikuyu kikamba kifaransa
kiswahili kikisii kijaluo
sheng kiluhya kikuria

(b)Kati ya lugha hizo ulizozitaja ni gani inayopendekezwa kutumiwa sana na wanafunzi?

Kiswahili
Sheng

2.(a) Je, sheng hupata Maneno yake kutoka lugha zingine?

Ndio

(b) Ikiwa unakubali, taja mifano ya Maneno hayo na maana zao katika Kiswahili

| Neno | maana |
|---|---|
| Masa | Mama |
| Buda | Baba |
| Mode | Mwalimu |
| bob | pesa |
| Muste | shule |

3(a) Je, Maneno ya Sheng huchukua miundo tofauti na ya Kiswahili?

Ndio

(b) Iwapo unakubali toa mifano

Masa – Mama
Buda – Baba
Fomu – Mlango
rada – chanjo
karao – polisi

4.(a) Je, Sheng huyapa Maneno ya Kiswahili maana mpya kando na maana ya kawaida?

ndio

(b)Kama unakubali toa mifano ya maneno hayo na maana yake ya ki-sheng.

| Neno | maana |
|---|---|
| Demu | Matambara / Msichana |
| Buda | kibogoyo / Baba |
| Masa | Maovu / Mama |
| Mbuyu | Mti / Baby |
| Dunga | Choma / vaa |
| Mhadhara | Shida / kikao cha usomi |

5.Je, kuna maneno ya sheng yaliyo na maana sawa?

Yataje

Doh, Mashiet -> pesa    Msupa, manzi - msichana

Toko, tenje -> simu

6.Je, kuna maneno ya sheng yaliyo na maana kinyume na mengine?

Yataje. Masa - Budg

Mathee - Fathee

Chali - Manzi

7.Je, kuna maneno ya sheng yaliyo na maana Zaidi ya moja?

Yataje

ndula, Maolipo -> viatu

8. Je sheng inaathiri vipi wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

- Kuchanganya Sheng na Kiswahili hasa katika Insha
- Kupotoka kisarufi
- Maongezi yasiyozingatia matamshi bora
- Ukosefu wa msamiati mwafaka wa kiswahili

9. Je, wewe kama mwalimu unaweza ukatambua makosa yanayotokana na sheng katika kazi ya mwanafunzi vipi?

Kusoma Insha zao

Kushiriki katika mazungumzo na wao

10. Makosa hayo unayarekebisha vipi?

- Kuhakiki kazi zao kwa makini na kuwarekebisha
- Kuwawekea vikwazo ili wasije wakazoea kutumia sheng kwa lugha ya kiswahili
- Kupigia kistari neno hilo kisha kumwandikia jibu sahihi

11. Je maoni yako ni yapi kuhusu suala nzima la sheng?

- Sheng imeathiri lugha ya kiswahili.
- Wanafunzi hutumia sheng katika uzungumzaji na uandishi.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

## KIAMBATISHO B. (VIELELEZO VYA INSHA)

(Kidato 1)

### SIKU YANGU YA KWANZA SHULENI

Siku tuliyokuwa tunaisubiri kwa hamu na ghamu ilikuwa imewadia
Niliamka asubuhi na mapema kisha nikaelekea kwa kisima huku nikiwa
na ndoo ya maji. Alafu nikajichukua maji kwa bafu kisha nikaoga.
Nilipomalisa kuoga nilifaa sare zangu za shule kisha nikapata
kiamsha kinywa. Wakati huo masa alikuwa amemalisa kujitayarisha
pia. tukaondoka. Punde si punde tulipanda teksi iliyokuwa tayari
na ikatufikisha kwa gate ya shule. Furaha ilinizidi moyoni
mwangu. Nilijaribu kujituliza lakini sikuweza Nilipiga nduru
kwa sauti yangu ya juu kabisa hadi watu walishangaa
nini niliyoona hadi nilipiga nduru. Masa yangu aliniulisa ni
nini lakini sikumjibu. Kuingia kwa gate tulimpata mlinzi
akatuambia tuandike majina yetu kwenye kitabu kidogo hivi
Tulipomalisa alituambia tuende mpaka kwa ofisi ya Princi
Kubisha tu sauti ilitukaribisha ndani nasi tukaingia. Princi
alitugotea na kutukaribisa vipoa. Alikagua kila kitu
tulichokibeba baada ya kutosheka aliandika jina langu
Jini na kumwita naibu wake Alimwamuru aliniisindi hadi
darasani. Kabla ya kuondoka masa alinipa noti ya ngiri
moja na ~~kis~~ kuishia. Viatu zangu zilikuwa zinangara zilinibeba
na heshima Nilikua na tengeneza nyumba kwa hewe nikifikiria
juu ya shule ya sekondari. Nilipofika darasani nilikaribishwa na
kiranja nika furahi sana. Niliketi na mwanafunzi aliyeitwa
Vincet Ouma. Alikuwa mpole na mwerevu. Tulikua marafiki
wazuri sana kwa siku hiyo. Waalimu walikuja na masomo
mpya kama vile biologia na mengi mengine. Saa ya mchezo
ilikuja wate wote walitoka inje nikabaki pekee yangu. Ndio
wanafunzi wa kidato cha nne walinionea. Walijakua pesa
yangu yote Nilienda kwa mwalimu, Mwalimu aliita wazazi
wao na kuwatoa nje ya shule. Siku yangu ilikua mbaya
sana Mwalimu alinipa pesa ya kutumia hadi mzazi
wangu atume zingine

F2

Kidato cha pili

Insha

# Siku ya Michezo Shuleni.

Siku tuliyokuwa tunaisubiri kwa hamu na ghamu ilikuwa imewadia. Niliamka asubuhi na mapema na kuanza shughuli za kujitayarisha kisha nikaondoka kwenda. Nilipata kiamshakinywa kisha nikaondoka kwenda chuoni. Ilikuwa siku ya Jumanne ambapo shule za kaunti yetu ya Kisii zingeshiriki katika michezo ya mipira. Michezo hii ingekuwa chuoni mwetu. Kutikia kwa gwande tulijisanja na kuomba bahara ipasavyo na kuchomoka hadi madarasani. Wanafunzi wengine hawakuweza kulicha adha yao kwa kucheleweshwa namna hiyo. Mmoja kimza hamzaha akasirika akinung'unika ya kwamba nguvu zake za kucheza zinaendelea kupunguka. Mzaha huo ukatua twa na kicheko kikubwa.

Mazee ilipotika saa nne ivi mastude kutoka chuo mbalimbali walianza kuingia na mandai yao makubwa makubwa. Kabla ya game kuanza mastude pamoja na mamode wao walikuwa wametunika uwanjani tundu. Walikuwa wamechangamka na kila mtu alikuwa na mudenge wake wakinong'onezana yasiyoweza kusikika na wengine.

Ghafla bin vuu mademu wa chuo jirani walipoingia maboiz wetu waliwadandia ju walikuwa supu sana. Lakini mimi siku hiyo sikubahatika hata sekunde moja. Nilisikia vibaya sana hata niliitamani siku hiyo iishe haraka nisiione tena maishani mwangu.

Kidogo ivi mwalimu mmoja alipuliza filimbi ili watu wamsikilize na kutumia kipasa sauti. Mwalimu huyu alisema kuwa michezo ilikuwa tayari kuanza na chuo yetu ilikuwa ianze kwa mchezo wa kandanda ya maboiz. Kusikia hivyo nilichangamka kiac kwa vile nilijua chuo yetu ingeshinda. Atta dakika chache kuisha game ikaanza. Baada ya dakika tisini game ikaisha huku tukiwa washindi

Game zingine ziliendelea vizuri lakini ilipotimia saa nane mawingu meusi yalitanda mbingu yote. Mara tu mvua ilianza kunyesha hadi saa kumi na mbili. Mvua ilipoisha kila mtu alianza kuondoka na michezo iliyosalia ikaahirishwa hadi kesho yake ndipo nikaamini kuwa kila kingáacho si dhahabu

Kidato 3

# SIKU YA AJABU

Siku tuliyokuwa tunaisubiri kwa hamu na ghamu ilikuwa imewadia. Miliamka asubuhi na mapema nikamwamsha buda pia ili tusue tukachelewa arusi hiyo ilikuwa tulijita arusi ya baba mdogo aliyeishi mjini Nakuru. Kwa vile masa alikuwa tarisho haraka haraka na kuondoka. Nilikuwa nimiji mgonjwa ilitubidi tuhudhurie na buda. Kwatua kwatu kwatu. Kutokana na umbali wa mahali tulikokuwa tunaenda, ilitubidi tutoke mapema bila hata kiamsha kinywa. Kufika kwa kituo cha magari tulipanda mat iliyokuwa kwanza na ikaondoka baada ya muda mfupi. Tulipokuwa kwa hiyo mat nilimcheka buda akinywa kitu nikadhani ni maji safari ilikuwa ndefu kwa vile nilikuwa na hamu ya kufika na kucheki mji wa Nakuru kwa mara yangu ya kwanza. Tulilala na kuamka na kupata safari inaendelea bado. Baada ya masaa matatu mat ilisimama na kondaa akasema mwisho wa gari. Watu walianza kushuka. Tuliposhuka kutoka kwa mat buda alionekana amechoka sana na akalala chini. Nilishtuka sana nikashindwa kwani amekuwa mgonjwa au nini. Kufungua macho kabla ya kuku kumeza punje ya mahindi nilichoki kufunga na ndai moja nyeusi pi ikiendeshwa na karao ikija upande wetu. Hiyo ndai ilikuwa mbio na kupiga breki mbele yetu. mavijana wakatokeleza huku wamejihami na mabundo na kuanza kukimbia tulikokuwa. Cijui niltoa miguu wapi nilikimbia mbio ambazo zingeweza kumshinda David Rudisha. Baada ya kukimbia maili kadhaa nilicheki nyuma na kumwona buda amebebwa hobelahobela na kurushwa kwa ndai ile. Ju singeweza kurudi nilizidisha mbio zangu na nikasimama mahali hakukuwa na watu wengi. Kwa vile sikuwa na nauli ya kurudi nyumbani na sikujua mjomba alikoishi. Nilimwona domu mmoja akipita nikamsalimu na kumwomba simu ili nimpigie masa home ili nikamwarifu yaliyojiri. Masa aliposikia vile alimpigia baba mdogo aliyekuwa bwana arusi na kumweleza hali yetu.

Baada ya saa moja kijana mmoja akaja nilikokuwa nimesimama. na kunisalimu. Akanishow kuwa baba mdogo amemtuma anipeleka kwa nyoma. Wakati huo nilikuwa sina furaha tena. Tulipofika

nyumbani nilipewa chakula nikala shingo upande na nikaelekezwa arusini ambayo tayari ilikuwa karibu kuisha. Arusi ilipoisha tulirudi nyumbani kisha baba mdogo akasema lazima tumfuate buda kwenye kituo cha polisi. Tulipofika kituoni makarao walituamrisha tulipe ngiri tano na baba mdogo akalipa. Tulipotoka kituoni tulirudi nyumbani na kweli hiyo ndiyo iliyokuwa siku ya ajabu maishani mwangu.

kidato 4

SIKU YA KUZALIWA KWANGU

Siku tuliyokuwa tunaisubiri kwa hamu na ghamu ilikuwa imewadia. niliamka asubuhi na mapema maze kujitayarisha. nilijikata kwenda kitchen ili nipate kiamsha kinywa. nilipata masa asha tayarisha chai, Lakini escort haiku masa alinigei anwani niendee escort. Afta kukudi nikatek breko alafu nikaenda bafu kuogelea.

Afta kumaliza niliwaambia ma-arif zangu twikale kwa vile buda alikuwa ampe ndai yake siku hiyo. ~~kwa hiyo vile~~ ma-arifu zangu walipokuja tulijikata na mimi ndiye nilikuwa dere-mazee kidogo ivi tulipata fom afta kuskia kuna sama tulia Launchi tulizid sha tu. Tulipofika tulia tukaingia ndani. Tulikombasha na kusombooshear alafu kidogo ivi tu~~#~~ makarao wakakam. Alafu progam ikaspoili niliudi ka ile mbaya. Nilikuwa nimetei jaani nilikua maji, hiyo singewéza kuitengeneza kwa ~~hiyo~~ vile mathao talikua yamesonga mbaya.

Tulipotoka pale tayari ilikuwa saa kumi na moja, ma arif zangu wakaniambia tuende tukadish kiac lakini nilisua buda ataleta noma kwa vile tulikua tumekubaliana kufika nyumbani mapema. Tulijikat kwenda home. Tulipoegesha gari mahali pake ma arifu zangu walinipa tuzawadi walizokua wameniletea na wakajikata.

masa alikua anapika kwa vile nilikua nimechoka sana nilijifululiza hadi kitandani hata sikutamani kula. siku hiyo nilibambika tu sana hata kama starehe zangu zilikatishwa na makarao. kwa kweli hiyo siku ilikuwa na raha na karaha kwangu.